www.umg.co.tz


*Leo yetu ndiyo kesho yetu*

# Mwelekeo



## KIMATAIFA
### Anglikana wamkataa Askofu Mkuu Welby

Habari ⇉ Uk.8



SIASA

UK.16

## ELIMU
### Idadi ya wanaokatisha masomo Sekondari za Ruangwa inatisha

Uk. 14



Toleo Na. 00002

| Jumatano Februari 22 - 28, 2023 |

umgdigital · umgdigital · mwelekeo@umg · YouTube umgdigital

# Dk. Samia afanya kweli Bondeni




Rais Dk. Samia Suluhu Hassan

Uk. 4

## HABARINDANI

### Ziara ya Wajumbe Sekretarieti ya NEC Tanga



Sophia Mjema

HABARI UK.5



### Daladala wapandisha nauli kinyemela

Uk. 4

# Filamu ya Royal Tour, Faru vyachochea utalii Mkomazi

**Mwandishi Wetu, Same**

KIVUTIO cha Utalii wa Faru katika Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi, kimetajwa kuwa moja ya vichocheo vikubwa vya kuongezeka kwa wageni wanaotembelea hifadhi hiyo.

Kichocheo kingine ni Filamu ya Royal Tour iliyotayarishwa mwaka jana ikiongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan.

Filamu hiyo ni maalumu kwa ajili ya kutangaza utalii ili kuwavutia watalii wa nje na ndani ya nchi pamoja na kutembelea hifadhi za taifa hapa nchini.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Hifadhi hiyo, Emmanuel Moirana, uboreshaji wa miundombinu katika hifadhi, pia umeongeza idadi ya watalii wanaotembelea hifadhi hiyo, iliyoko katika mikoa ya Kilimanjaro na Tanga.

> **Hili ni ongezeko la karibu asilimia 100 kwa mwaka mmoja na kama nilivyosema, limetokana na sababu hizo kubwa tatu...**

Akizungumza na waandishi wa habari waliotembelea Mkomazi hivi karibuni, Moirana alisema ongezeko hilo la watalii pia limesababisha kuongezeka kwa mapato. Alisema mwaka 2021/2022, watalii 6,324 wakiwemo 4,827 wa ndani walitembelea hifadhi hiyo ikilinganishwa na watalii 3,238 wakiwemo 2,677 wa ndani waliotembelea hifadhi mwaka 2020/2021.

"Hili ni ongezeko la karibu asilimia 100 kwa mwaka mmoja na kama nilivyosema, limetokana na sababu hizo kubwa tatu.

"Filamu ya Royal Tour imehamasisha sana watalii, kuboreshwa kwa miundombinu ya hifadhi ikiwa ni pamoja na barabara, ukarabati wa viwanja viwili vya ndege na utalii wa Faru ambao hapa kwetu unapatikana kwa namna ya kipekee vimechangia sana," alisisitiza.

Alisema hata makadirio ya idadi ya watalii kwa mwaka 2022/2023, yamevuka malengo kwa zaidi ya asilimia 100 hadi kufikia Januari, mwaka huu ambapo wageni 5,785 wakiwemo watalii 4,129 wa ndani, wametembelea hifadhi.

"Kutokana na kasi ya ongezeko la wageni, tunakadiria kuwa hadi kufikia mwisho wa mwaka huu wa fedha, idadi ya watalii watakaofika Mkomazi, itafikia 10,000.

"Pamoja na kumshukuru na kumpongeza Rais Samia kwa Filamu ya Royal Tour, pia tunatoa shukrani za dhati na kupongeza uongozi mzima wa TANAPA chini ya Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini, Jenerali Mstaafu George Waitara na

Kamishna Uhifadhi, William Mwakilema kwa sera, mipango na maelekezo sahihi ya kuimarisha mifumo na taratibu za utekelezaji wa majukumu ya shirika," alisema.

Kwa mujibu wa Moirana, wageni wengi wanaotembelea hifadhi hiyo wanatoka mataifa ya Ujerumani, Ufaransa, Uhispania na Marekani. Kuhusu uboreshaji miundombinu hasa ya barabara, Moirana alisema jumla ya kilomita 146 za barabara na vivuko vitano vimekarabatiwa.

Alisema barabara na vivuko hivyo sasa vinapitika katika kipindi chote cha mwaka.




**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo, akikata utepe wakati wa uzinduzi wa Kitabu cha Maarifa ya Asili katika Uhifadhi wa Mazingira, kilichoandaliwa na Taasisi ya Wanahabari ya MAIPAC. Wengine kutoka kushoto ni Meneja Miradi MAIPAC, Debora Makando, Mratibu wa Programu Miradi Midogo ya Mfuko wa Mazingira Duniani (GEF) katika Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Faustine Ninga, Katibu Tawala Msaidizi Daniel Loiruki na Mkurugenzi wa MAIPAC, Mussa Juma. (Picha: Mpigapicha Wetu)**

## Zaidi ya shule 300 nchini kunufaika mafunzo ya ICT

**Na Mwandishi Wetu, Lindi**

WANAFUNZI wa zaidi ya shule 300 za sekondari kote nchini, watanuifaka na mafunzo ya somo la teknolojia na mawasiliano, yanayotarajiwa kuendeshwa kwa ushirikiano wa taasisi tatu.

Taasisi hizo ni African Child Project, Vodacom Tanzania na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF), lengo likiwa ni kuziwezesha shule hizo kufundisha somo la ICT.

Chini ya mpango huo, Vodacom Tanzania na UCSAF wanatoa vifaa zikiwemo kompyuta na viambatanishi ili vifungwe katika shule wakati African Child, itaratibu mradi huo unaotekelezwa hadi visiwani Zanzibar.

Shule 21 zinakazonufaika na mpango huo katika hatua ya awali, zipo mkoani Lindi na saba katika hizo zipo wilayani Nachingwea, tano Liwale, sita za Wilaya ya Mtama na tatu wilayani Kilwa.

Mmoja wa waratibu wa mradi huo wa kipekee kutoka African Child, Athuman Msangi, alisema kabla ya kuzifika shule zote nchini na kuzipa vifaa hivyo, zilitembelewa ili kuona kama zina miundombinu inayoweza kutumika kwa ajili ya somo hilo.

Alisema viongozi wa mashirika rafiki kote nchini, wamekuwa wakitembelea shule hizo na kwamba pamoja na mambo mengine, wamekuwa wakifuatilia kwa karibu uwepo wa vyumba kwa ajili ya somo la ICT, walimu wenye taaluma na utayari wa walimu hao katika kuendesha mafunzo.

Ofisa Elimu Taaluma wa Mkoa wa Lindi, Kulwa Masaya alisema kama malengo ya mradi huo yatatimia, itasaidia kuleta mabadiliko chanya kwa wanafunzi kwa kuzingatia kuwa dunia sasa imetawaliwa zaidi na mifumo ya kiteknolojia.

Shule za sekondari zinazotarajiwa kunufaika na mradi huo mkoani Lindi ni pamoja na Nambambo, Shule ya Wasichana ya Nachingwea, Shule ya Sekondari ya Kutwa ya Nachingwea, Kipaumbele, Naipanga na Naipingo zote za Wilaya ya Nachingwea.

Katika Wilaya ya Kilwa, ni Shule za Sekondari za Ilulu, Kilwa na Mpunyule wakati katika Wilaya ya Liwale ni Likongowele, Rashid Mfaume Kawawa, Liwale, Nangano, Anna Magoa na Kibutuka.

## Waandishi wahimizwa kuzingatia weledi

**Na Mwandishi Wetu, Mwanza**

WAANDISHI wa habari nchini, wametakiwa kufanya kazi zao kwa weledi na kwa kuzingatia maadili ili kuimarisha umoja, amani na utulivu kwa manufaa ya taifa. Rai hiyo ilitolewa hivi karibuni na Mkuu wa Kitengo cha Habari katika Ubalozi wa Marekani hapa nchini, Michael Pryor, alipokuwa akizungumza katika mafunzo kwa waandishi wa habari.

Mafunzo hayo kuhusu matumizi ya teknolojia na zana za kisasa, yaliwahusisha waandishi wa habari wa Mkoa wa Mwanza.

Alisema dunia sasa imejikita katika matumizi ya teknolojia ya juu inayojumuisha pia zana za kisasa katika sekta mbalimbali ikiwemo ya habari na kwa hiyo, waandishi lazima wawe na ufahamu wa kutumia zana hizo ili hatimaye, wazitumie vema katika utendaji wa kazi zao.

Pryor alisema vyombo vya habari ni muhimili muhimu katika kuharakisha maendeleo ya watu na taifa kwa jumla na kwa msingi huo, lazima vifanye kazi kwa huru na bila kupendelea upande wowote.

"Tunaamini kwamba ili nchi iwe na demokrasia yenye nguvu, lazima kuwe na vyombo huru vya habari ambavyo utendaji wake unapaswa kuzingatia maadili. Kwa maana ya kuripoti habari za pande zote bila upendeleo, kutumia vyanzo vingi vya habari, kuchunguza, kuthibitisha na kujumuisha takwimu," alinena Pryor. Mkuu huyo wa habari katika Ubalozi wa Marekani, alisema jambo hilo ndilo lililousukuma Ubalozi kuona umuhimu wa kushirikiana na Muungano wa Klabu za Waandishi wa Habari Nchini (UTPC), kutoa mafunzo kwa waandishi wa Mkoa wa Mwanza.

Alisema zana za kisasa katika nyanja ya habari, zinarahisishha mno utendaji, lakini lazima kuwe na uangalifu mkubwa katika matumizi yake, ili kuepuka kupotosha habari zinazohusu maisha ya watu na kusababisha migongano katika jamii.

Kwa upande wake, Mtaalamu wa Habari katika Ubalozi wa Marekani, Japhet Sanga, alisema uandishi wa habari umebadilika na kuelekea kwenye mitandao, jambo linalowalazimisha waandishi wa habari nao kubadilika huku wakiendelea kuzingatia misingi ya taaluma yao.

"Maadili ni muhimu sana,

# Bodi ya Vileo Zanzibar kuwekwa `kitimoto'

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA) imesema itawaita viongozi wa Bodi ya Vileo Zanzibar (ZLB) kueleza wanavyosimamia vileo vinavyoingizwa kwa msamaha wa kodi ili kusimamia kama ilivyokusudiwa.

Hayo yalielezwa na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya ZAECA, Ali Abdallah Ali, alipozungumzia tuhuma za kuwepo kwa biashara ya magendo ya vileo kwa kampuni moja ya visiwani hapa kupitia taasisi moja ya ulinzi na usalama Zanzibar.

Ali alisema suala la kudhibiti magendo na kuwepo kwa mianya ya ukwepaji kodi, ipo taasisi husika inayosimamia majukumu hayo, lakini hata hivyo, ZAECA itawaita viongozi wa Bodi ili kufahamu wanavyosimamia bidhaa zinazoingizwa Zanzibar kwa misamaha ya kodi bila ya kuathiri ukusanyaji wa mapato na kuibuka magendo.

"ZAECA inafuatilia kwa karibu tuhuma hizo, hivyo tutawaandikia barua ya wito viongozi wa Bodi ya Vileo watuambie jinsi wanavyosimamia bidhaa zinazoingizwa Zanzibar na kunufaika na msamaha wa kodi na kuhakikisha zinatumika kama ilivyokusudiwa," alisema.

Akizungumza na waandishi wa habari, Kaimu Meneja wa Elimu ya Mlipa Kodi wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA), Makame Khamis, alisema kampuni tatu ndizo zilizopewa vibali vya kuingiza vileo kutoka nje ya Zanzibar tangu kuanza kutumika Sheria ya Vileo ya mwaka 2020.

"Kampuni zenye kibali cha kisheria kuingiza vileo Zanzibar ni One Stop Center, SCOCH , ZMMI na kampuni nyingine za vileo zilizosajiliwa kisheria. Kampuni nyingine Zanzibar zinapaswa kununua vileo kutoka kampuni hizo na kusambaza kwa wateja wao," alisema Makame.

Aidha, alisema tatizo la magendo litadhibitiwa Zanzibar iwapo wananchi wazalendo watashirikiana na vyombo vyenye dhamana vinavyosimamia kodi na udhibiti wa magendo kuhakikisha wanatoa mapema taarifa za siri kabla biashara haramu ya magendo kufanyika.

"Wito wangu kwa wananchi tunawataka wawe tayari kusaidia kutoa taarifa za siri mepema dhidi ya watu wanaojihusisha na biashara za magendo. Makusanyo ya kodi ndiyo msingi wa maendeleo kwa nchi zote duniani ikiwemo Zanzibar," alisema Makame.

# Mwarobaini wa matumizi ya kuni, mkaa waandaliwa

**Mwandishi Wetu, Arusha**

KATIKA jitihada za kupunguza matumizi ya kuni na mkaa, serikali inaandaa utaratibu mpya wa kudhibiti matumizi ya nishati hiyo, kwa kuanzia katika taasisi za umma.

Taasisi za umma ambazo bado zinatumia kuni na mkaa kama nishati ya kupikia, ni pamoja na magereza, vyuo vya elimu ya juu na kati, hospitali, vituo vya afya, zahanati na shule mbalimbali nchini. Hatua hiyo itasaidia kukabiliana na athari za ukataji misitu kwa ajili ya kupata nishati ya kupikia. Uharibifu wa mazingira umekuwa ukichangia athari za mabadiliko ya tabianchi ambazo zimesababisha mvua kupungua na hivyo kuathiri uchumi, uzalishaji wa umeme, kilimo na ufugaji nchini.

Waziri wa Nchi, Ofisi na Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Dk. Seleiman Jafo (pichani), alitoa mkakati huo hivi karibuni jijini hapa wakati akizindua Kitabu cha Maarifa ya Asili katika Uhifadhi wa Mazingira. Kitabu hicho kimeandaliwa na Taasisi ya Wanahabari ya MAIPAC.



Dk. Jafo alisema ukataji miti unaoendelea katika maeneo mbalimbali nchini kwa ajili ya kupata mkaa na kuni, utaendelea kudhibitiwa na serikali ili kutunza mazingira.

"Hivi karibuni, serikali itatoa utaratibu wa udhibiti wa matumizi makubwa ya kuni na mkaa katika taasisi zake ikiwa ni pamoja na magereza, shule na vyuo," alisema.

Alisema uharibifu wa mazingira umeanza kusababisha kupungua kwa uzalishaji wa mazao ya chakula ukiwemo mchele na kusababisha bei kupanda kutoka wastani wa kati ya Sh 1,500 na 2,000 hadi kufikia wastani ya kati ya Sh. 2,500 na 3,500.



**Mtetezi wa Haki za Wasichana, Mesha Singolyo (wa nne kushoto), akiwa katika picha ya pamoja na wanafunzi wa kidato cha kwanza baada ya kuwapa msaada wa vifaa vya shule katika Tarafa ya Sale Wilaya ya Ngorongoro mkoani Arusha hivi karibuni. Watoto hao walichelewa kujiunga shule za bweni walizopangiwa kwa takriban wiki tatu hadi waliposaidiwa vifaa hivyo. (PICHA: MPIGA PICHA WETU)**

# Waliokwama kuingia kidato cha kwanza `wapigwa jeki'

**Na Mwandishi Wetu, Arusha**

WASICHANA 55 wa jamii za wafugaji walioshindwa kujiunga na masomo ya kidato cha kwanza katika Wilaya ya Ngorongoro mkoani Arusha, wamesaidiwa vifaa na mahitaji muhimu vya kuwawezesha kuanza masomo.

Kwa hatua hiyo, wasichana hao kutoka Tarafa ya Sale, wilayani humo sasa wana uhakika wa kuanza masomo, japo kwa kuchelewa.

Mwanaharakati za Haki za Watoto wa Kike, Mesha Singolyo, alisema uamuzi wa kuwapatia msaada wasichana hao ulikuja baada ya wazazi kushindwa kuwanunulia vifaa kutokana na kukosa uwezo.

"Wazazi wa watoto hao wanategemea mifugo kwa kila kitu katika maisha yao, lakini kutokana na ukame, mifugo mingi ilikufa na hivyo kukosa uwezo wa kuwanunulia vifaa na mahitaji muhimu ya shule," alisema Mesha.

"Mabadiliko ya tabianchi yameathiri sana wafugaji ambao mifugo ndiyo tegemeo lao pekee la kiuchumi. Kwa hiyo tumeona ni busara tukawasaidia hawa wasichana ili waende kuanza masomo yao ya kidato cha kwanza japo wamechelewa kwa zaidi ya mwezi sasa," alisisitiza.

Mesha ambaye ni mwanaharakati anayeongoza kampeni ya kupinga ndoa za utotoni katika jamii za wafugaji, alisema vifaa na mahitaji waliosaidiwa wasichana hao ni pamoja na mablanketi, magodoro, ndoo za kuchotea na kuhifadhia maji, madaftari makubwa, kalamu na taulo za kike kulingana na mahitaji ya shule za bweni.

Akizungumza wakati wa makabidhiano ya vifaa hivyo, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro, Mohamed Bayo pamoja na kumshukuru Mesha kwa msaada huo, alitaka watu wengine katika jamii kuiga mfano huo kwa sababu ni muhimu kwa faida ya jamii na taifa zima.

"Msaada huu umekuja wakati unahitajika sana hasa ikizingatiwa kuwa watoto hawa kutoka familia maskini wamechelewa kuripoti shule kwa kukosa vifaa na mahitaji muhimu baada ya wazazi kukosa uwezo,mifugo yao iliathiriwa sana na ukame uliotukumba," alisema Mwenyekiti.

"Tunapaswa kuiga mfano wa mwanaharakati huyo (Mesha) ambaye amekuwa mstari wa mbele kupigania haki ya elimu kwa mtoto wa kike hasa wanaotoka katika jamii za wafugaji," alisisitiza.

Akizungumza katika makabidhiano hayo, Mesha ambaye anatoka katika jamii ya wafugaji, alisema aliamua kutoa msaada huo ili kuwaokoa wasichana hao kutoka katika hatari ya kuingia ndoa za utotoni ambazo wazazi wao wanaweza kushawishika kupokea mahari baada ya athari za ukame.

"Msaada huu si kwa ajili ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi tu, lakini pia kuwaokoa wasichana hawa ambao wanaweza kujikuta katika ndoa za utotoni kwa kuwa vishawishi ni vingi hasa wanapokuwa nyumbani bila kufanya shughuli yoyote ya maana," alinena Mesha.

"Kwa mila na desturi za wafugaji, watoto wa kike hawapewi kipaumbele katika elimu, na athari za mabadiliko ya tabianchi yanawaweka katika tishio kubwa la kuingia katika ndoa za utotoni kwa kuwa wazazi wanashawishika kubadilishana wasichana wao na mifugo katika mfumo wa mahari ili wazazi wamudu ugumu wa maisha,jambo tunalopaswa kulipiga vita kwa pamoja," alisema Mesha.

Jamii za wafugaji katika Wilaya za Ngorongoro, Longido na Monduli mkoani Arusha ambazo zinategemea mifugo kama uchumi wao, zimeathiriwa sana na ukame uliosababisha mifugo kufa kwa kukosa malisho na maji na kulazimisha wengi kuhama hama kutafuta malisho kwa ajili ya mifugo yao.

> **Huyu Mwenyekiti, ndiye aliyekuwa akitoa vibali vya marehemu wengine wazikwe katika maeneo ya maziko ya familia zao, inakuwaje sisi atukatalie?**

# Dk. Samia afanya kweli Bondeni

Na Mwandishi Wetu

NDOTO za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, kuhusu kuvutia uwekezaji mkubwa na wa kisasa katika sekta ya kilimo ndani ya Bonde la Mto Rufiji, Pwani, zimeanza kutimia.

Tayari maeneo ya ardhi ya vijiji 828 vilivyoko ndani ya bonde hilo, yamekwishapimwa ukiwa ni utekelezaji wa agizo la kiongozi huyo la Desemba 22, mwaka jana, kupitia hotuba yake ya uzinduzi wa ujazaji maji ndani ya Bwawa la Mwalimu Nyerere.

Katika hotuba yake, Dk. Samia alizitaka wizara kadhaa ndani ya serikali anayoingoza, kupima maeneo ya ardhi ya Bonde la Mto Rufiji, ili yatumike kwa shughuli za kilimo kikubwa na cha kisasa, ukiwa ni sehemu ya mikakati ya kuliwezesha taifa kujitosheleza kwa chakula.

Katika hotuba yake, Rais alisema Mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere, unakwenda kufungua fursa nyingi kwa Watanzania ikiwa ni pamoja na kilimo cha uhakika cha umwagiliaji, utalii katika Hifadhi ya Nyerere, uvuvi wa kisasa na udhibiti wa mafuriko ya mara kwa mara katika Mto Rufiji,

"Kwa hiyo, nitoe maelekezo mahususi kwa wahusika katika Wizara za Kilimo, Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na ile ya Mifugo na Uvuvi, najua kuna ekari 400,000 katika eneo la chini ya delta, maeneo hayo yakapimwe kwa ajili ya mashamba makubwa na yawekwe kwenye mnada," alisema Rais Dk. Samia.

Mnada huo wa maeneo ya kilimo, unalenga katika kuwapata wawekezaji wakubwa watakaoendesha miradi mikubwa ya kilimo cha kisasa ndani Bonde la Mto Rufiji na kuliwezesha taifa kuwa na uhakika wa chakula.

Rais Samia ambaye amekuwa akifanya jitihada kubwa ya kutekeleza miradi ya kimkakati, alitaka hatua za kupima maeneo hayo zifanyike sambamba na za kuwasaidia wakulima wadogo wadogo wa maeneo ya Bonde la Mto Rufiji, kuhakikisha kuwa maeneo yao nayo yanapimwa.

Akizungumza na Mwelekeo kwa njia ya simu hivi karibuni, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula, alisema upimaji wa maeneo yaliyoanishwa unaendelea na kwamba unafanywa kwa awamu.

> **Kuna vijiji kama 3,035 vinavyozunguka eneo la Bwawa la Mwalimu Nyerere tunavyopaswa kuvipima. Tayari tumeshapima vijiji 828 na zoezi linaendelea, wapimaji wanakwenda hatua kwa hatua...**

"Kuna vijiji kama 3,035 vinavyozunguka eneo la Bwawa la Mwalimu Nyerere tunavyopaswa kuvipima. Tayari tumeshapima vijiji 828 na zoezi linaendelea, wapimaji wanakwenda hatua kwa hatua," alisema Dk. Mabula.

Alisema upimaji huo unafanywa na maofisa wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi kwa kushirikiana na wenzao wa Mamlaka za Hifadhi za Taifa (TANAPA).

Kauli hiyo ya Waziri imekuja siku 60 kamili tangu Dk. Samia alipotoa agizo lake, hali inayoashiria kasi ya haraka ya watu wa timu yake, katika kupokea na kutekeleza maagizo.

Sehemu kubwa ya maeneo ya vijijini vilivyoko katika mpango wa kupimwa, vinapakana na Hifadhi ya Taifa ya Mwalimu Nyerere.

"Kwenye maeneo yanayopakana na hifadhi, Wizara ya Maliasili na Utalii inachangia na tunashirikiana na TANAPA," alisema.

Baadhi wananchi wa Rufiji, wameelezea kufarijika kwao na mpango huo wa serikali kwa maelezo kwamba utasaidia mno uzalishaji wa chakula nchini na kuliwezesha taifa kujiwekea akiba ya chakula.

"Naamini kama kutakuwa na wawekezaji wa uhakika na wakajitokeza kwa haraka ili kuendesha kilimo cha kisasa katika Mto Rufiji, Tanzania itapiga hatua kubwa sana katika suala la chakula." alisema Khamis Mkosa.

Mkosa ambaye alizungumza kwa simu kutoka Nyamwage wilayani Rufiji, alisema hatua hiyo si tu kwamba italifanya taifa liwe na uhakika wa usalama wa chakula, lakini pia itatoa fursa za ajira kwa vijana wa Rufiji na maeneo mengine ya nchi.

Mkosa alisema hata hivyo, serikali inapaswa kuhakikisha kuwa uwekezaji mkubwa katika sekta za kilimo na uvuvi ndani ya Mto Rufiji, unawahusisha pia Watanzania badala ya wawekezaji wa kigeni pekee yao.

Kwa upande wake, mkazi wa Ndundu, Fadhili Mtambe, alisema uendeshaji wa shughuli za kilimo kikubwa na cha kisasa katika Bonde la Mto Rufiji, utachangia mno jitihada za serikali za kuhakikisha kuwa Tanzania inajitosheleza kwa chakula.

Kwa sasa, shughuli za kilimo cha mazao katika mto huo mkubwa, zinafanywa kwa kutumia zana duni na hivyo kutokuwa chenye tija katika mipango ya serikali ya kujitosheleza kwa chakula.

Hali kadhalika, Mto Rufiji umekuwa ukikumbwa na mafuriko ya mara kwa mra yanayosababisha mazao ya kilimo kuharibiwa vibaya.

Kwa mujibu wa Rais, Bonde la Mto Rufiji lifungua pia fursa za uvuvi na utalii wa kisasa kwa wananchi wa maeneo hayo.



Mto Rufiji



# Daladala wapandisha nauli kinyemela

Na Mwandishi Wetu

NAULI za mabasi ya daladala katika baadhi ya njia jijini Dar es Salaam, zimepanda kinyemela na kwa kiwango kikubwa kiasi cha kuibua malalamiko kutoka kwa wananchi wanaotumia usafiri huo wa umma.

Mabasi ambayo wafanyakazi wake wamepandisha nauli hizo kiholela, ni yale yanayotoa huduma zake kutoka pembezoni kwenda katikati ya Jiji la Dar es Salaam, hususani Gerezani Kariakoo.

Uchunguzi wa Mwelekeo kuhusu kadhia hiyo, umebaini kuwa nauli za daladala zimepanda kwa karibu mara mbili ya nauli ya kawaida.

Baadhi ya njia ambazo mabasi yake yamepandisha nauli hizo ni za Tegeta Nyuki-Kariakoo, Mbagala-Kariakoo, Kisemvule-Kariakoo, Toangoma-Kariakoo, Kisewe-Kariakoo na Gongo la Mboto-Kariakoo.

Nauli halali katika njia hizo kwa safari, ilikuwa haizidi Sh. 850, lakini sasa imefikia Sh. 1,300 kwa ama kwenda au kurudi Kariakoo.

Hata hivyo, hakuna mabadiliko ya viwango vya nauli yaliyofanyika kwenye tiketi za abiria na hata maandishi kuhusu nauli yaliyoko karibuni na milango ya mabasi, yanayohalalisha nauli. Hali hiyo anaashiria kuwa upandaji wa nauli hizo unafanywa kinyemela na bila ridhaa ya mamlaka iliyopewa jukumu la kusimamia usafiri wa ardhini.

Uchunguzi umebaini kuwa nauli hizo zinatozwa zaidi nyakati za asubuhi na jioni ambapo wafanyakazi wa daladala, wamekuwa wakitengeneza mazingira yanayosababisha uchache wa mabasi na kuwalazimisha abiria kulipa nauli mara mbili.

Kwa mfano, mabasi yanayotoka Kisemvule, Mbagala, Kigamboni au Kisewe zinapofika nyakati hizo, hukatisha njia katika eneo la Kamata na hivyo kuwalazimisha abiria waliopaswa kuyapanda wakiwa katika Kituo Kikuu cha Gerezani, kuyafuata na hatimaye kulipa Sh. 1,300 ili wageuke nayo.

Uchunguzi wetu umebaini kuwa ukiukwaji wa kanuni hizi za usafirishaji, ulianza kidogo kidogo mwishoni mwa mwezi uliopita na sasa umekithiri na hivyo kuibua malalamiko kutoka kwa wananchi wanaotegemea usafiri wa daladala kwenda na kurudi kwenye shughuli zao za kila siku.

Kero hiyo imekuja huku kukiwa na malalamiko ya watu kuhusu kupanda kwa bei ya bidhaa na hasa za vyakula mbalimbali, jambo linalosababisha maisha kwao kuwa magumu zaidi.

Baadhi ya watu waliozungumza na gazeti hili, wamezitaka mamlaka zinazohusika kuchukua hatua dhidi ya wenye daladala zinazokiuka taratibu na hivyo kuwasababishia wananchi maisha magumu. "Tunashangaa nauli za daladala zinapanda kiholela na hakuna maelezo yanayotolewa na mamlaka za serikali kuhusu kero hii.. Ongezeko la Sh. 450 kwa safari ya Sh. 870 kutoka Kisemvule-Gerezani, Kigamboni au Kisewe, si pesa ndogo hata kidogo. Tunataka wahusika watueleze kwa nini inakuwa hivi," alisema Jeramiah Ludidi.

Ludidi alisema kupanda kinyemela kwa nauli hizo, ni kuwabebesha wananchi mzigo mkubwa zaidi katika maisha yao ya kila siku na kwamba ni vema serikali ikachukua hatua za haraka kukomesha kero hiyo.

Alipotakiwa kuzungumzia kupanda kwa nauli hizo, Msemaji wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), alisema yuko Morogoro na kwamba hakuwa katika nafasi nzuri ya kuzungumzia jambo hilo.

Lakini wakati hayo yanaendelea, mamlaka hayo yametangaza njia mpya ya mabasi kutoka katika maeneo ya pembezoni mwa Jiji ambako kuna makazi mapya.

Taarifa ya LATRA kupitia tovuti yake, imewataka wasafirishaji kuomba leseni kwenye njia hizo mpya ambazo ni kutoka Kibada Stendi, Kigamboni kwenda Mbezi Luis, Simu 2000, Temeke Mwisho, Tabata Segerea, Tegeta Nyuki na Kigogo Sokoni.

Ilisema mabasi yatakayoomba njia hiyo, yataanzia safari zake na kuishia Kibada Stendi kupitia Kivuko cha Daraja la Nyerere.

Kwa mujibu wa taarifa, magari yatakayofanya safari za Mbezi Luis na Simu 2000, yatapita Daraja la Nyerere hadi Barabara za Mandela na Morogoro wakati zitakazoelekea Tegeta Nyuki, zitapita Darajani, Mandela, Sam Nujoma hadi Bagamoyo.

Ruti ya Temeke kwa mujibu wa LATRA, magari yatapitia Daraja la Nyerere hadi Barabara ya Kilwa na yale yanayoelekea Kigogo Sokoni, yatapita Barabara ya Mandela na hatimaye Barabara ya Nyerere.

Njia nyingine ni kutoka Pugu Stesheni hadi Kawe kupitia Barabara za Nyerere, Uhuru na Kawawa.

Hali kadhalika, njia ya kutoka Bunju Sokoni hadi Kawe Ukwamani, Tegeta Nyuki-Kawe Ukwamani, Kigogo Sokoni-Temeke, Kwa Lugwadu – Mbagala Rangi Tatu na kutoka Hospitali ya Vijibweni kwenda Muhimbili, Machinga Complex, Mnazi Mmoja, Makumbusho, Simu 2000, Kawe Ukwamani na Tabata Segerea. Mamlaka inawataarifu wasafirshaji kuwa imetengeneza na kuidhinisha njia mpya za mabasi ya mjini kwa Mkoa wa Dar es Salaam…njia hizi zinategemea kuongeza wigo wa uwekezaji katika usafirishaji wa umma na utoaji huduma kwa wananchi," ilisema sehemu ya taarifa.

# Ziara ya Wajumbe wa Sekretarieti ya NEC mkoani Tanga

**Februari 18, mwaka huu, Wajumbe wa Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), walifanya ziara ikiwa ni utekelezaji wa Ilani ya Chama katika Wilaya ya Handeni mkoani Tanga. Zifuatazo ni nukuu za baadhi ya viongozi hao walipotembelea na kukagua Hospitali ya Wilaya ya Handeni ya Handeni Islam Health iliyopo Mkata wilayani humo.**

**NUKUU:**

**Katibu wa Halmashauri ya CCM ya Taifa Itikadi na Uenezi, Sophia Mjema.**



**1**

**"DMO tumeongea naye pale mpaka mwisho wa mwezi huu, watu waanze kutibiwa hapa."**

**2**

**"Kwa ubora wa jengo hili la Mama na Mtoto la hospitali hii, tumpongeze sana Mheshimiwa Rais."**

**3**

**"Nimuagize Meneja TANROADS Mkoa wa Tanga aje ahakikishe alama zote za tahadhari zimewekwa katika barabara hii ya kuingilia ili kuepuka ajali."**

**NUKUU:**

**Katibu wa Oganaizesheni, Issa Haji Usi Gavu.**



**1**


**"Kwa huduma hizi za afya zilivyoboreka, sasa ni raha ya uzazi kwa mama maana uchungu wa mwana haipo tena kwa sababu ya huduma bora."**

**2**

**"Tuko Handeni ikiwa na muendelezo wa ziara za ukaguzi wa utekelezaji wa Ilani, hakika tunampongeza sana Mheshimiwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, Mwenyekiti wetu kwa kazi kubwa sana anayoifanya."**

**3**

**"Kama mlivyoahidi, huduma zianze ili wananchi wapate huduma hapa."**




**Wajumbe wa sekretarieti hiyo, walitangazwa mapema mwaka huu.**
**Wajumbe hao ni Katibu Mkuu ameendelea kuwa Daniel Chongolo, Naibu Katibu Mkuu Bara, Annamringi Macha, Naibu Katibu Mkuu Zanzibar, Mohemed Said Dimwa. Aidha, Katibu Itikadi na Uenezi ni Sophia Edward Mjema, Katibu wa Idara ya Uchumi na Fedha, Dk. Frank Hawasi, Katibu Siasa na Uhusiano wa Kimataifa, Mbarouk Nassoro na Katibu wa Oganaizesheni, Issa Haji Usi Gavu.**

# Maoni ya Mhariri & Uchambuzi

**HII NI KERO**



## Ukosefu wa maji Mbezi Luis

**NI wiki ya pili sasa na ushee, wakazi wa Mbezi Luis Mtaa wa Makondeni wanataabika kutafuta maji ambapo kina Mama Lishe, vijana na kina mama wa nyumbani, wanapita kila kona kutafuta maji kwa ajili ya kupikia na matumizi mengine muhimu ya nyumbani. Mbaya zaidi, jana watu wa mtaa huo, wamejikuta wakitumiwa bili za maji wakikumbushwa kulipia mwezi huu wa pili ambao tangu uanze, maji hayajatoka katika mabomba yao yanayoonekana kukauka kama vile hayajawahi kutoa maji.**




**MAONI YA MHARIRI**

## Utoro shule za sekondari muhimu utafutiwe dawa

KUMEKUWA na tabia kwa baadhi ya wanafunzi wa shule za sekondari nchini, kukatisha masomo bila ya sababu za msingi, jambo ambalo ni hatari kwa ustawi wao na taifa kwa ujumla.

Mathalani, katika toleo letu hili la leo Februari 22, mwaka huu ukurasa wa 14, kuna makala yenye kichwa habari `Idadi ya wanaokatisha masomo Sekondari za Ruangwa inatisha.'

Kwa mujibu wa makala hiyo, Wilaya ya Ruangwa mkoani Lindi, imeonyesha kuwa na mafanikio makubwa katika kujenga shule za sekondari.

Hili linatokana na ukweli kwamba, mwaka 2007, wilaya hiyo ilikuwa na shule za sekondari mbili tu, lakini hadi kufikia mwaka huu, tayari ina shule za sekondari 24. Haya ni mafanikio makubwa katika kipindi cha takriban miaka 15.

Hata hivyo, pamoja na mafanikio hayo ya ongezeko la shule za sekondari, zipo taarifa zisizofurahisha za utoro uliokithiri kwa wanafunzi wa sekondari katika wilaya hiyo.

Makala hiyo inatueleza kwamba, hadi kufikia mwishoni mwa mwaka jana, jumla ya wanafunzi 224 kati ya 522 kutoka katika shule sita tu kati ya 12 zilizotembelewa wilayani humo, wameacha masomo.

Takwimu hizi zinaonyesha kwamba, asilimia 47 takriban nusu ya wanafunzi walioanza kidato cha kwanza kati ya mwaka 2019 hadi mwaka 2020, wamekatisha masomo. Hakika, takwimu hizi zinatisha.

Kana kwamba hiyo haitoshi, uchunguzi uliofanywa na Mwelekeo kwa miezi kadhaa, umebaini kuwa tangu mwaka 2019, idadi ya wanafunzi wanaokatisha masomo imekuwa ikiongezeka taratibu kila mwaka na sasa inakaribia nusu.

Mwelekeo limekuwa likifuatilia maendeleo ya wanafunzi hao na hali ya ufaulu kwa karibu katika shule 12 za Wilaya ya Ruangwa na sita kati ya hizo zimetoa jibu la kuwepo kwa changamoto hiyo.

Hata hivyo, hakuna sababu ya moja kwa moja inayotolewa kuhusu kinachochangia wanafunzi wengi kukatisha masomo, ingawa baadhi ya wazazi na walezi wamedai kuwa kushindwa kufuatilia maendeleo ya kila siku ya wanafunzi ni mojawapo ya sababu.

Wazazi wanapaswa kushirikiana kwa karibu na walimu kuhakikisha kwamba watoto hao hawapati mwanya wa kutoroka shuleni kwa kuwa wakishatoka huko, bila shaka huripoti majumbani kwao.

Hivi ni mzazi gani usiyemhoji mwanao unayemuona karejea nyumbani bila sababu ya msingi? Hapana, wazazi Ruangwa badilikeni na muwadhibiti watoto wenu wazingatie masomo.

**UMGL MEDIA** Wasiliana nasi

**Mhariri Mkuu:** +255713263775 / +255748115000
**Mhariri wa Habari:** +255693257410 / 0766005061
**Mhariri Michezo:** +255713055011 / 0621350860
**Meneja Masoko/Biashara:** + 255718480406 / + 255733768825
**S. L. P:** 15110, Dar es Salaam
**Makao Makuu Mtaa:** Barabara ya Morogoro
**Jengo la:** Aura Mall
**Chumba Cha Habari:** +255 (0)222151532
**Email:** jaridalamwekeleo@gmail.com



Na Dk. Felician Kilahama
**WAZO BINAFSI**
fkilahama@gmail.com

# Wezi vifaa vya miradi wasionewe huruma

MWANZONI mwa mwaka huu, Jeshi la Polisi lilitoa taarifa kuhusu matokeo ya operesheni ya kubaini na kukamata wezi wa mafuta na vifaa vya ujenzi kwenye mradi wa Reli ya Kisasa (SGR) kipande cha Isaka - Mwanza.

Operesheni hiyo ilifanywa kwa kushirikiana polisi wa Mikoa ya Mwanza, Shinyanga na Simiyu.

Akizungumza kwa niaba ya Makamanda wa Polisi Mikoa ya Shinyanga, Simiyu, Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Mwanza, SACP Wilbroad Mutafungwa, alisema kamwe hawapo tayari kuona mradi huo unahujumiwa na baadhi ya wafanyakazi waliopo ndani ya mradi huo na wananchi walio nje ya mradi huo.

Kamanda Mutafungwa alisema Jeshi la Polisi katika mikoa ya Shinyanga, Simiyu na Mwanza wanaendelea na msako mkali na operesheni ya pamoja ya kuwabaini na kuwakamata watu wote wanaohujumu ujenzi wa mradi huo wa Reli ya Kisasa kwa namna yoyote iwe kuiba,kupokea, kushiriki kuiba mafuta na vifaa vingine vya ujenzi.

Katika taarifa yake hiyo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, SACP Mutafungwa alisema polisi mkoani humo wamekamata lita 4,426 za mafuta ya aina dizeli na petroli na pia watu tisa wametiwa mbaroni kwa tuhuma za makosa mbalimbali likiwemo la wizi wa vifaa katika mradi wa SGR.

Kamanda Mutafungwa alisema pia polisi walifanikiwa kukamata mifuko 646 ya saruji aina ya Huaxin na bomba 28 za vyuma zinazodhaniwa kuwa mali za mradi SGR unaojengwa toka Isaka mkoani Shinyanga hadi Mwanza.

Kadhalika, alisema polisi walikamata pikipiki tatu moja aina ya Sun LG yenye namba ya usajili MC 507 BCY, nyingine aina ya King Lion yenye namba za usajili MC 199 DMN na ya tatu pia aina ya King Lion ambayo plate namba yake iliondolewa na watuhumiwa hao kwa lengo la kutofahamika wakati wakitekeleza uhalifu.

Kwa mujibu wa Kamanda Mutafungwa, operesheni hiyo ilianza Januari 11, mwaka huu katika vijiji vya Isunga, Nkalalo-Bukwimba, Malya na Usagara wilayani Kwimba na Misungwi.

Aidha, Jeshi la Polisi mkoani Mwanza, limeendelea kuwaomba wananchi kutoa ushirikiano ili kuwadhibiti wezi hao wenye malengo ya kurudisha nyuma maendeleo ya taifa.

Serikali imekuwa ikijitahidi kubuni na kutekeleza miradi mbalimbali kwa lengo la kuweka mazingira wezeshi kwa wananchi wake.

Kinachotakiwa ni uaminifu mkubwa katika kufanya kazi kwa faida ya mhusika na taifa kwa ujumla; lakini siyo kujihusisha na wizi wa vifaa, udanganyifu au kuharibu miundombinu.

Mbali na mradi wa SGR, serikali pia imekuwa ikitekeleza miradi mingi ikiwemo ya barabara, maji; nishati, elimu na afya.

Tangu taifa lipate Uhuru Desemba 9, mwaka 1961; nguvu nyingi zimekuwa zikielekezwa katika eneo la miradi hiyo.

Ni dhahiri serikali imejitahidi kiasi cha kutosha ingawa hatupaswi kubweteka bali tunahitaji kukaza 'mwendo kwa kasi kubwa zaidi.'

Kwa msingi huo, hakuna sababu ya kuwaonea huruma wala haya, wote wanaohujumu miradi ya serikali na badala yake wanaothibitika kutenda kosa hilo, wapewe adhabu kali kwa mujibu wa sheria ili liwe funzo kwa watu wengine wenye nia kama hiyo.

# Majaliwa akerwa wafugaji kulisha mifugo mashambani

**Na Abdul Mitumba, Ruangwa**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewaonya wafugaji wanaomiliki idadi kubwa ya mifugo, kuacha mara moja mtindo wa kuingiza na kulisha mifugo yao kwenye mashamba ya wakulima wilayani Ruangwa.

Mara kadhaa katika baadhi ya maeneo hapa nchini, mtindo huo ambao Majaliwa amesema haukubaliki, umekuwa ukiibua migogoro na hata mapigano kati ya wakulima na wafugaji.

Majaliwa alitoa onyo na maelekezo hayo hivi karibuni alipokuwa akizungumza na wananchi katika Kijiji cha Narungombe, muda mfupi baada ya kuzindua jengo la Kituo cha Afya cha kata hiyo.

"Ukiwa na mifugo mingi hata wakati wa malisho, utaanza kuona shida. Wewe mwenyewe upo hapa, lakini mifungo yako imetangulia mbali na huko hujui kama inakula mazao ya watu mashambani au la," alisema Waziri Mkuu.

Aidha, Majaliwa aliwaagiza viongozi wa vijiji kuhakikisha kuwa kila mfugaji anayeingiza mifugo wilayani humu, anakuwa na idadi ndogo ya kumudu kuwalinda na kuwalisha ipasavyo bila kuwaingiza kwenye mashamba ya wakulima.

Kwa mujibu wa Waziri Mkuu, vitendo vya baadhi ya wafugaji kumiliki idadi kubwa ya mifugo wasiyoweza kuidhibiti wakati wa malisho, imekuwa ikisababisha migogoro isiyokuwa ya lazima kati ya wakulima na wafugaji. Alisema Tanzania ni nchi huru ambayo inampa kila mtu uhuru wa kwenda popote na kuishi, ili mradi utaratibu uliowekwa uzingatiwe ikiwa ni pamoja na viongozi wa serikali za vitongoji na vijiji kuwatambua wageni ili kuweka rekodi sawa.

Katika kufanikisha hilo, amewaagiza viongozi wa vitongoji na vijiji kuwa macho na kuratibu idadi ya wafungaji wanaoingia kwenye maeneo yao na kuratibu mifugo ili kuhakikisha wanakuwa na wastani ya mifugo.

"Sambamba na yote, viongozi wa vijiji na kata, hakikisheni mnatenga maeneo ya malisho kwa wafugaji na maeneo sahihi kwa ajili ya kilimo. Mkifanya hivyo mapema wananchi wenu mtawanusuru na migogoro ya wakulima na wafugaji," alisema.



Waziri Mkuu na Mbunge wa Ruangwa, Kassim Majaliwa, akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Mary Majaliwa, wilayani Ruangwa baada ya kukagua ujenzi wa bweni la wasichana shuleni hapo jana. (Picha: Ofisi ya Waziri Mkuu).

## DC awatolea uvivu wasioajiri mgambo

**Na Abdul Mitumba, Ruangwa**

UONGOZI wa Serikali wilayani Ruangwa, umezitaka kampuni na taasisi binafsi kuwaondoa mara moja kazini, walinzi wasiokuwa na sifa na nafasi zao zichukuliwe na askari mgambo waliohitimu mafunzo yao mwishoni mwa mwaka jana.

Pia uongozi huo umewaagiza watendaji wa vijiji kuhakikisha kuwa katika awamu ijayo ya mafunzo, wanawapeleka mafunzoni vijana kutoka vijijini.



Agizo hilo lilitolewa hivi karibuni na Mkuu wa Wilaya ya Ruangwa, Hassan Ngoma (pichani), alipokuwa akizungumza katika sherehe za kuhitimu mafunzo kwa wanamgambo 108 wa wilaya hiyo. Mafunzo hayo yaliyodumu kwa wiki 16, yaliwashirikisha vijana 90 wa kiume na wengine 18 wa kike.

"Naagiza hapa kwamba, kampuni binafsi za ulinzi, ziache kuajiri askari wasiopitia mafunzo ya mgambo na ni marufuku kuanzia sasa kuajiri askari na kuwapunja misharahara.," alisema.

DC Ngoma alisema hapendi kuona au kusikia lindo moja linalipwa Sh.300,000 kwa mwezi, lakini askari anaambulia Sh.100,000 au chini yake.

"Nataka walipwe kuanzia Sh. 200,000 na kuendelea," alisema DC Ngoma na kusisitiza kuwa kuwalipa kiasi kidogo askari ni kuwaingiza kwenye majaribu ya kutokuwa waaminifu.

Maagizo hayo yalifuatia malalamiko ya wanamgambo hao kwa serikali kuhusu kutoajiriwa hata pale zinapotokea fursa.

"Na hapa nataka kuwaambia wahitimu wetu kwamba mbali na ajira katika sekta binafsi, pia tunazo nafasi nyingi kwenye majeshi yetu ya Polisi, Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ), Jeshi la Zimamoto, Uokoaji, Uhamiaji na kadhalika. Huko kote kunahitajika watu waliopitia kwanza mgambo," alisema.

Akizungumzia utaratibu uliotumika kwa watu kujiunga na mafunzo JKT, DC Ngoma alisema, mwaka uliopita, Wilaya ya Ruangwa ilipata nafasi 50 za kupeleka vijana JKT, lakini ni watu 45 tu ndiyo waliokidhi vigezo.

"Nawaomba, askari wote mliohitimu sasa na wale wenye sifa za kujiunga JKT, kuandaa viambatanisho vyote muhimu ikiwemo cheti cha kuzaliwa, kitambulisho cha Taifa au Namba za NIDA. Pia hakikisha unajitunza ili mwili usiwe na makovu au alama za Tatuu mwilini," alisema.

## Mtendaji atuhumiwa kutafuna michango

**Na Mwandishi Wetu, Ruangwa**

OFISA mmoja wa serikali Wilaya ya Ruangwa mkoani Lindi, anatuhumiwa kutafuna kiasi cha Sh. milioini 3.4 za michango ya wananchi wa vijiji viwili zikiwa katika mchakato wa kupelekwa benki. Fedha hizo ambazo ofisa huyo amekiri kuzipokea, zilichangwa na wananchi wa Vijiji vya Juhudi A na B katika Kata ya Chingongwe wilayani Ruangwa.

Habari zilisema kiasi hicho cha fedha, ni sehemu ya zaidi ya Sh. milioni 8.2 zilizokusanywa na Kamati ya TASAF kutoka kwa wananchi maskini katika vijiji sita vya Kata ya Chingongwe.

Fedha hizo zimetokana na michango ya kuwawezesha wananchi hao kusajiliwa katika utaratibu wa kupata huduma ya matibabu kupitia Mfuko wa Afya ya Jamii Vijijini (CHF).

Taarifa ambazo gazeti hili imezipata mjini hapa, zilimtaja mtendaji anayekabiliwa na tuhuma hizo kuwa ni Mohamed Makota.

> **Hata hivyo, namshukuru Mungu, nimeanza kulipa deni hilo na tayari nimetoa Sh. 930,000. Nikivuna ufuta nitamaliza kulipa deni hilo...**

Hata hivyo, katika mazungumzo yake kwa njia ya simu na mwandishi wa habari hizi, Makota alikiri kukabidhiwa fedha hizo, lakini alikanusha tuhuma kuwa amezitafuna kinyume cha taratibu.

Alidai kuwa fedha hizo zimeibwa na watu waliovamia nyumba yake wakati akiwa safarini kwenda kapata huduma za matibabu nje ya kijiji hicho.

Makota alisema pamoja na fedha hizo, wezi hao pia waliiba televisheni na vitu vingine kadhaa kutoka kwenye nyumba yake.

"Hata hivyo, namshukuru Mungu, nimeanza kulipa deni hilo na tayari nimetoa Sh. 930,000. Nikivuna ufuta nitamaliza kulipa deni hilo," alisema Mtendaji Makota.

Habari zilisema zoezi la kukusanya michango hiyo na kumkabidhi mtuhumiwa, lilisimamiwa na Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Kata ya Chinongwe, Novath Kweka. Akiibua tuhuma hizo, Mwenyekiti wa Kijiji cha Juhudi B, ambaye wakati fedha hizo zinachangwa alikuwa akikaimu pia uongozi katika Kijiji cha Juhudi A, Japhari Lwidi, alisema kupotea kwa fedha hizo, kumeibua malalamiko kutoka kwa wananchi.

Lwida alitoa tuhuma hizo alipokuwa akizungumza katika semina ya mafunzo ya utawala bora yanayoratibiwa na Jukwaa la Elimu ya Uraia Tanzania na kushirikisha wenyeviti na watendaji wa vijiji, watendaji wa kata, madiwani na wenyeviti wa kamati tatu za kudumu za vijiji vyote.

Mradi huo uliozinduliwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa Aprili, mwaka jana, umefadhiliwa na Shirika la Kimataifa la Ujerumani la Hanns Seidel Foundation (HSF) lenye ofisi zake jijini Dar es Salaam.

# Maaskofu Anglikana duniani wamkataa Askofu Mkuu Welby

**LONDON, Uingereza**

KUNDI la viongozi wa Kanisa la Kianglikana kutoka sehemu mbalimbali duniani, wamemkataa Askofu Mkuu wa Canterbury, Justin Welby, kuwa kiongozi wao baada ya Kanisa la Uingereza kuunga mkono maombi ya baraka kwa wapenzi wa jinsia moja.

Maaskofu wakuu wanaowakilisha majimbo 10 kati ya 42 katika Ushirika wa Kianglikana, wametia saini taarifa wakisema hawamfikirii tena Welby “ kuwa kiongozi wa ushirika wa kimataifa.”

Waliongeza kuwa Kanisa la Anglikana “lilikataliwa” kama “Kanisa Mama” lao la kihistoria.

Ni mara ya kwanza kwa uongozi wa Askofu Mkuu wa Canterbury kukataliwa na kundi kubwa la makanisa.

Tangu ilipoanzishwa mwaka wa 1867, Askofu Mkuu aliyoko madarakani wa Canterbury, amechukua nafasi ya kiongozi wa kiroho wa Ushirika wa Kianglikana ambao ni ushirika wa kimataifa wa Makanisa 42 ya Kianglikana.

Hata hivyo, hana mamlaka rasmi badala yake, ana mamlaka ya kimaadili na anaonekana kama “wa kwanza kati ya walio sawa.

Lambeth Palace, makao rasmi ya Askofu Mkuu wa Canterbury, ilisema hakuna mabadiliko rasmi katika muundo wa Ushirika wa Anglikana yanayoweza kufanywa bila idhini kutoka kwa “vyombo” vyake vinne vya utawala.

Kanisa la Uingereza linaunga mkono mipango ya kubariki ndoa za wapenzi wa jinsia moja.



Maaskofu wakuu 10, pamoja na wawili kutoka majimbo ya kihafidhina yaliyojitenga nchini Marekani na Brazili, wanapinga kubariki au kuolewa kwa wapenzi wa jinsia moja.

Wanaunda sehemu ya wanachama wa kikundi kiitwacho Global South Fellowship of Anglican Churches (GSFA), ambacho kinadai kuwakilisha asilimia 75 ya Waanglikana duniani kote, hasa kote Asia na Afrika.

Waliotia saini ni pamoja na Mwenyekiti wa GSFA, Askofu Mkuu Justin Badi wa Sudan Kusini na maaskofu wakuu wa Chile, Bahari ya Hindi, Congo, Myanmar, Bangladesh, Uganda, Sudan, Alexandria na Melanesia.

Askofu mkuu wa kanisa la Uganda, Stephen Kaziimba, alisema: ‘Mungu hawezi kubariki kile anachokiita dhambi.

Katika taarifa ya Jumatatu walisema “hawana uwezo tena wa kumtambua Askofu Mkuu wa sasa wa Canterbury kama kiongozi sawa wa kwanza kati ya viongozi sawa wa ushirika wa kimataifa”.

“Kanisa la Uingereza limechagua kuvunja ushirika na majimbo hayo ambayo yanasalia kuwa waaminifu kwa imani ya kihistoria ya kibiblia,” taarifa hiyo ilisema.

> **Kanisa la Uingereza limechagua kuvunja ushirika na majimbo hayo ambayo yanasalia kuwa waaminifu kwa imani ya kihistoria ya kibiblia...**

Baada ya mjadala mkali uliodumu kwa zaidi ya saa nane, Baraza Kuu la Kitaifa la Sinodi Kuu, lilipiga kura kwa kura 250 kwa 181 kuunga mkono pendekezo la maaskofu lililokusudiwa kumaliza miaka mingi ya migawanyiko na kutoelewana ikiwemo Kuhusu mapenzi ya jinsia moja.

Mapema mwezi huu, Kanisa la Uingereza, ambalo linaongozwa na Welby, liliidhinisha maombi ya baraka kwa wapenzi wa jinsia moja kwa mara ya kwanza.

Hata hivyo, msimamo wake kuhusu ndoa za wapenzi wa jinsia moja haujabadilika na wapenzi wa jinsia moja bado hawataweza kufunga ndoa kanisani.

Mipango hiyo, iliyowekwa na maaskofu mwezi uliopita, imekosolewa na wale wanaodhani wanaenda mbali zaidi na wale wanaodhani hawaendi mbali vya kutosha.

Msemaji wa Ikulu ya Lambeth alisema “inathamini kikamilifu” msimamo wa GSFA, lakini akaongeza “kutoelewana kwa kina” kati ya Waanglikana juu ya kujamiiana na ndoa ni ya muda mrefu na kwamba mageuzi katika jimbo moja hayaathiri sheria katika maeneo mengine.

“Katika ulimwengu wa migogoro, mateso na kutokuwa na uhakika, lazima tukumbuke kuwa zaidi hutuunganisha kuliko kutugawanya.

“Pamoja na tofauti zetu, lazima tutafute mbinu za kuendelea kutembea na kufanya kazi pamoja kama wafuasi wa Yesu Kristo ili kuwahudumia wenye uhitaji,” walisema.

**BBC**



## wanajeshi 51 wauawa Burkinafaso

**OUAGADOUGOU, Burkina Faso**

WANAJESHI wasiopungua 51 wa Burkina Faso, wameuawa katika shambulizi la kushtukiza lililotokea eneo la Kaskazini mwa nchi hiyo.

Mashambulizi hayo yametokea katika eneo linalofahamika kwa hujuma kubwa za makundi ya itikadi kali za dini.

Taarifa iliyotolewa jana na Jeshi la Burkina Faso, ilieleza kuwa wanajeshi hao walishambuliwa kwenye Jimbo la Oudalan ambalo linaitenganisha nchi hiyo na taifa jirani la Mali.

Shambulizi hilo ambalo linatajwa kuwa limesababisha idadi kubwa ya vifo vya wanajeshi kwa wakati mmoja tangu kuzuka kwa uasi wa makundi ya itikadi kali nchini humo, limetokea siku mbili kabla ya Ufaransa kuhitimisha operesheni zake za kijeshi nchini humo.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa mkasa mwingine uliotokea kwenye jimbo lingine la Kaskazini mwa nchi hiyo, wanamgambo wenye silaha wamewateka nyara wanawake 50 waliokuwa msituni kutafuta chakula.

Kufuatia utekaji huo, serikali imetangaza msako wa wanamgambo hao ili kuokoa wanawake wasiokuwa na hatia.

**DW**

# Kinshasa, Kigali wazidi kukorofishana

**KIGALI, Rwanda**

UHUSIANO wa kidiplomasia kati ya Serikali za Kinshasa na Kigali, bado ni kizungumkuti, jambo linaloashiria kuwepo kwa ugumu zaidi katika jitihada za kuzipatanisha pande hizo mbili.

Katika mgogoro huo, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) imekuwa ikiishutumu Rwanda kwa kile inachodai kuwa ni kuwasaidia waasi wa Kundi la M23, katika vitendo vyao vya kuvamia maeneo ya nchi hiyo na kuzorotesha usalama wa raia na mali zao. Hata hivyo, mara kwa mara, Rwanda imekuwa ikikanusha tuhuma hizo na badala yake, inaituhumu DRC kwamba imekuwa


Rais Tshisekedi


Rais Kagame

ikiwasaidia waasi wa FDLR (Watutsi) waliokimbia nchini humo baada ya mauaji ya Kimbari ya mwaka 1994, kuendelea kuihujumu (Rwanda).

Mapema wiki hii, Rwanda ilimshutumu Msemaji wa Serikali ya DRC, Patrick Muyaya, kwa kile kilichodaiwa kuwa ni kulihalalisha kundi la waasisi la FDLR.

“Patrick Muyaya (Msemaji wa Serikali ya DRC), amekielezea kikundi cha waasi cha FDLR kuwa ni chama chenye uhalali na sababu za kupigania inachokipigania,” imedaiwa. Inadaiwa kuwa Muyaya alitoa tuhuma hizo alipokuwa akizungumza na Kituo cha Televisheni cha Aljazeera.

Mamlaka za mjini Kigali zimedai kuwa kauli hiyo, sasa imeweka hadharani msimamo wa muda mrefu na ambao DRC imekuwa ikiuficha kuhusu FDLR.

Habari zinasema msimamo huo pia umekuja siku kadhaa baada ya Rais Felix Tshisekedi kusema kwamba Wanyarwandwa wanahitaji kusaidiwa ili kuleta mabadiliko ya kiungozi nchini mwao.

Rwanda inadaiwa kuwa FDRL ambayo sasa inashirikishwa katika Jeshi la Congo, imekuwa ikijitapa hadharani kuwa bado ina kazi ya kumalizia nchini Rwanda.

Rwanda inadai kuwa kazi hiyo ni ya kuwaua Watutsi na kwamba ilianza kwa kuwaua katika maeneo ya Kaskazini mwa DRC . Huku serikali yao ikiwa inaangalia tu, M23 iliamua kuchukua mtutu wa bunduki ili kujitetea, lakini leo serikali inakiita kitendo cha kujitetea kwao kuwa ni ugaidi.

Wakati huo huo, mchambuzi wa masuala ya kisiasa nchini Rwanda, Dk. Lonzen Rugiza, amedai kuwa kitendo cha Serikali ya DRC kukihalalisha kikundi cha waasi wa FDLR, ni ushahidi wa wazi kuwa inakitumia kama gari la Rais Tshisekedi la kwenda kutekeleza sera za serikali yake nchini Rwanda.

*Leo ndiyo, kesho yetu*

Mweleko

JARIDA

# Jungu kuu

Jumatano Februari, 22-28, 2023




**Jarida hili haliuzwi**




UK. 12 & 13

# Rais Samia ameonyesha ukomavu, kazi kwenu wapinzani jengeni hoja



UK. 13

## Rais Samia anavyozidi kuneemesha Tanzania

## Kujisahihisha kwa kiongozi si kujidhalilisha

UK. 16



Uchumi



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, akiwa pamoja na mwenyeji wake, Rais wa Jamhuri ya Watu wa China, Xi Jinping, wakati wa ziara yake nchini humo hivi karibuni.

# Rais Samia anavyozidi kuneemesha Tanzania

**Mwandishi wetu**

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan, amekuwa katika mstari wa mbele kuitengeneza Tanzania yenye ushirikiano na utengemano na mataifa mengine duniani ili hatimaye, kuharakisha maendeleo.

Ziara kadhaa alizozifanya katika nchi kadhaa hivi karibuni na kusaini mikataba mbalimbali ya kimaendeleo, ndizo zinazodhihirisha namna kiongozi huyo alivyopania kuijenga Tanzania katika nyanja mbalimbali zikiwemo za kiuchumi na kisiasa.

Ziara hizo ni pamoja na ile ya China aliyoifanya kati ya Novemba 2 hadi 4, mwaka mwaka jana

Ziara hiyo kwa Rais Dk. Samia, ilifuatia mwaliko wa Rais wa Jamhuri ya Watu wa China, Xi Jinping na ilikuwa ya kwanza kufanywa na kiongozi wa juu kutoka Bara la Afrika tangu kiongozi wa China achaguliwe tena na Mkutano Mkuu wa 20 wa Chama cha Kikomunisti cha China kuwa Katibu Mkuu wa chama hicho kwa muhula wa tatu.

Katika ziara hiyo, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia alishuhudia utiaji saini wa Mikataba na Hati 15 za Makubaliano ya kimkakati. Alishuhudia hati hizo akiwa na mwenyeji wake Rais Xi Jinping.

Mikataba hiyo iliyolenga kuimarisha ushirikiano wa kibiashara na uwekezaji kati ya nchi hizo mbili, ni pamoja na ule uliohusu China kuipunguzia Tanzania sehemu ya deni lake la thamani ya Sh.bilioni 31.4.

Mikataba mingine ya kimkakati ni pamoja na makubaliano yaliyotiwa saini kuhusu mahitaji ya kuwepo kwa soko kubwa la usafirishaji wa maparachichi kutoka Tanzania kwenda China. Mkataba huo una manufaa makubwa kwa wafanyabiashara wa maparachichi ambao watapata fursa ya kuuza matunda hayo nchini China.

Pia kulisainiwa makubaliano kuhusu mahitaji ya kuwepo kwa soko kubwa la Usafirishaji wa mabondo ya samaki pamoja na bidhaa nyingine za uvuvi kutoka Tanzania kwenda China.

Chini ya makubaliano hayo, wafanyabiashara wa Tanzania wanaojihusisha na uuzaji wa samaki, watanufaika kwa kusafirisha samaki kutoka hapa nchini kwenda China.

Pamoja na kuzungumza na mwenyeji wake, Rais Dk. Samia pia alizungumza na Waziri Mkuu wa China na Spika wa Bunge la nchi hiyo.

Lakini pia Rais Samia ambaye pia ni Mwewnyekiti wa CCM alifanya ziara nyingine nchini Misri ambako alikutana na Rais wa nchi hiyo, Abdel Fattah El-Sisi katika mji wa Sharm El Sheikh.

Katika ziara hiyo, viongozi hao walizungumzia masuala mbalimbali yanayohusu uhusiano na ushirikiano kati ya nchi hizo mbili hasa kuwepo kwa mikakati mahsusi ya kuongeza kasi ya biashara na uwekezaji kati ya Tanzania na Misri. Viongozi hao walizungumzia ujenzi wa mradi wa kufua umeme wa Julius Nyerere unaojengwa na wakandarasi kutoka Misri na kuonyesha kuridhishwa na kasi ya ujenzi wa mradi huo.

Katika mazungumzo yao, viongozi hao walisisitiza umuhimu wa kuutekeleza

> **Katika ziara hiyo, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia alishuhudia utiaji saini wa Mikataba na Hati 15 za Makubaliano ya kimkakati...**

mradi huo kwa ubora na viwango vya uhakika hata kama utachelewa nje ya muda uliotarajiwa hapo awali.

Pia Marais hao walisisitiza kuwa timu ya wataalamu wa pande zote mbili, wafanye kazi kwa karibu ili kutatua changamoto ndogo ndogo zinazojitokeza kwenye mradi huo.

Mafanikio ya mradi huo ni pamoja na kuongeza nguvu ya nishati umeme katika sekta mbalimbali nchini Tanzania ikiwa ni pamoja na sekta ya viwanda, migodi na sekta nyingine.

Katika mkutano huo, Rais Dk. Samia aliongozana na Waziri wa Nishati, January Makamba, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Stergomena Tax na Balozi wa Tanzania nchini Misri, Dkt. Emmanuel Nchimbi. Rais Dk. Samia, pia alifanya ziara ya kiserikali nchini Qatar ambako alishuhudia utiaji saini wa makubaliano ya ushirikiano kati ya Chemba ya Biashara ya Tanzania, Zanzibar na Chemba ya Biashara ya Qatar.

Kwa upande wa Chemba ya Biashara ya Tanzania, mkataba ulisainiwa na Rais wa Chemba hiyo, Paul Koyi na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Kitaifa wa Wafanyabiashara Zanzibar (ZNCC), Ali Suleiman Amour.


Lengo la mkataba huo ni kuimarisha biashara na uwekezaji kati ya wafanyabiashara wa Tanzania na Qatar hususan kwenye sekta za utalii, miundombinu, ujenzi wa mahoteli na usambazaji wa gesi.

Mbali na utiaji saini huo, Rais Samia alifanya mazungumzo na Waziri wa Fedha wa Qatar, Ali bin Ahmed Al-Kuwari ambapo walijadili masuala ya kikodi baina ya nchi hizo mbili katika sekta za uwekezaji, biashara, gesi, ufugaji, utalii na kilimo ili kutengeneza mazingira ahueni ya utozaji tozo kwa wafanyabiashara.

Katika kuboresha sekta ya afya, Rais Dk. Samia na Waziri wa Afya wa Qatar, Dkt. Hanan Mohamed Al Kuwari, walikubaliana kuwa wataalamu kutoka Tanzania na wa Qatar, wabadilishane uzoefu kwenye sekta hiyo hasa katika huduma za kibingwa na za dharura.

Katika ziara hiyo ya kikazi, Rais Dk. Samia alifanya mazungumzo na Amiri wa Qatar, Sheikh Tamim bin Hamad al Thani, wafanyabiashara wakubwa na kuhudhuria Mkutano wa Ubunifu wa Afya Duniani (World Innovation Summit for Health) kwa malengo ya kuboresha na kuimarisha sekta ya biashara na afya.

Hizo ni baadhi ya ziara zenye mafanikio makubwa ambazo Rais Dk. Samia alizifanya.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, akiwa na Kiongozi wa Taifa la Qatar, Sheikh Tamim bin Hamad Al Thani, mara baada ya kuwasili kwenye ofisi za kiongozi huyo hivi karibuni.

Siasa

Na Lauden Mwambona, Songwe

# CCM Songwe ilivyojipanga kulinda majimbo yote 2025

MKOA wa Songwe, umeundwa na kuanza rasmi majukumu yake mwaka 2016. Kwa maneno mengine, uliundwa baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 uliofanyika wakati karibu eneo lote la ardhi linalouunda, likiwa Mkoa wa Mbeya.

Wilaya zilizochukuliwa kutoka Mbeya ili kuunda mkoa huu mpya ni za Ileje na Mbozi, wakati Wilaya ya Chunya ilimegwa kipande ambacho sasa kinaitwa Wilaya ya Songwe ndani ya Mkoa wa Songwe.

Wilaya ya Ileje imebaki na eneo lake lote likiwa ndani ya Mkoa wa Songwe, lakini Wilaya ya Mbozi imegawanywa katika wilaya za Mbozi na Momba.

Kisiasa, kabla ya kuundwa kwa Mkoa wa Songwe, Wilaya ya Mbozi ilijulikana kama Ngome ya Upinzani kwa sababu majimbo matatu ndani ya wilaya hiyo, yalinyakuliwa na upinzani mwaka 2015.

Mwenyekiti Mstaafu wa CCM wa Wilaya ya Mbozi ambaye alianza kazi yake mwaka 2017 na kumaliza mwaka 2022, Kapteni Mstaafu Simon Mboya, anasema wakati ule Mkoa wa Mbeya ambao ulikuwa na majimbo 12, ulipoteza majimbo matano yakiwemo matatu kutoka Wilaya ya Mbozi.

Majimbo yaliyochukuliwa na upinzani katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, ni Mbozi Magharibi, Tunduma na Momba na kwamba kipindi hicho, kata 11 zilichukuliwa na upinzani, zikiwa sehemu ya kata 29 za Mbozi.

Hata hivyo, mara baada ya kuundwa kwa Mkoa wa Songwe mwaka 2016, CCM ilijipanga vizuri na hatimaye mwaka 2017, ikapata viongozi waanzilishi wa CCM wa Mkoa na Wilaya mpya za Songwe na Momba.

Mboya anasema majimbo ya sasa ni Ileje, Momba, Tunduma, Songwe, Vwawa na Mbozi ambayo yanapaswa kulindwa kwa mbinu zote ili yaendelee kubaki mikononi mwa CCM.

Naye Mwenyekiti Mstaafu wa CCM Wilaya ya Songwe, Mwalimu Hamad Juma ambaye ni mwanzilishi wa Ofisi za CCM wilaya hiyo, anasema kwa kipindi cha miaka mitano, CCM imeweza kuhamasisha kila kata ipate eneo la ofisi, ofisi ya wilaya na hata ofisi ya mkoa.

Anasema hadi sasa eneo itakapojengwa Ofisi ya CCM Mkoa limeshapatikana kwa ushirikiano wa viongozi wa CCM na serikali.

Mwenyekiti wa kwanza wa CCM mkoa huo, ni Ellyniko Mkolla ambaye ameongoza kwa miaka mitano hadi mwaka 2022.

Mkolla anasema mara baada ya kushika wadhifa, aliamua kuisimamia kikamilifu Katiba ya CCM hasa ibara ya 5 kifungu kidogo cha 1 Katiba ya 1977 kinachoanisha malengo makuu ya chama cha siasa, amabyo ni pamoja na kushinda uchaguzi wa serikali za mitaa na Uchaguzi Mkuu.

Anasema akiwa na viongozi wenzake wa mkoa, wilaya hadi kwenye mashina, walishirikiana kuweka mikakati na kuwarudisha wakazi wa Songwe kwenye Chama sahihi na njia sahihi ya maendeleo.

"Mwaka 2020 ulifanyika uchaguzi mkuu na hapo ndipo tulipoamua kufanya kazi kwa vitendo na ushirikiano wa hali ya juu na hatimaye majimbo yote matatu yalirudi CCM Kata 32 zote zilirudi CCM," anasema.

Anakipongeza Chama chake kwamba kilimteua Waziri Mkuu Mstaafu, Mizengo Pinda kuwa mlezi wa CCM Mkoa wa Songwe na kwamba amefanya kazi kwa ufanisi wa hali ya juu.

Anasema uongozi wa CCM mkoa chini ya mlezi wake, Mzee Pinda ndiyo uliourudisha Mkoa wa Songwe kwenye rangi ya kijani.

Mkolla anawapongeza pia viongozi wa serikali ngazi ya mkoa na wilaya waliopita na waliopo akisema kwamba wamefanikisha malengo ya CCM na kuifanya iaminiwe na wananchi. Anasema ahadi ya CCM kwa wananchi kupitia Ilani ya uchaguzi ya mwaka 2020 ni pamoja na kudumisha utu, umoja, haki na mshikamano wa taifa ili kuleta utulivu wa nchi.

Ilani hiyo pia inasema CCM itaendeleza uchumi wa kisasa na kujenga miundombinu shirikishi ,uchumi imara, miongoni mwa jamii na kutoa huduma bora kwa jamii hususan za afya, elimu, maji ,barabara na matumizi sahihi ya teknolojia.

Katika kutekeleza hayo, serikali ndiyo inayosimamia na anasema kwa bahati nzuri, serikali kupitia taasisi zake imefanya mambo mengi mazuri.

Mwenyekiti mstaafu kwa niaba ya viongozi wenzake waliostaafu, anashauri viongozi wa sasa CCM kwa kila ngazi, wawaeleze wananchi miradi iliyopo katika maeneo yao ili waielewe.

> **Mwaka 2020 ulifanyika uchaguzi mkuu na hapo ndipo tulipoamua kufanya kazi kwa vitendo na ushirikiano wa hali ya juu na hatimaye majimbo yote...**

Mkolla anasema miradi ni mingi na Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, imetoa fedha nyingi sana ambazo lazima wananchi wanataka kujua namna zilivyotumika.

Kauli hiyo inaungwa mkono na Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Waziri Kindamba ambaye anasema Serikali inayoongozwa na Rais Dk. Samia hadi ilipofika Februari mosi, mwaka huu, imeleta Sh. bilioni 36.6 kwa ajili ya sekta ya afya mkoani Songwe.

Kindamba anasema kana kwamba haitoshi, serikali imetoa Sh. 2.5 bilioni kwa ajili ya sekta ya barabara, Sh bilioni 20.2 kwa ajili ya maji na Sh bilioni 8.1 kwa ajili ya sekta ya elimu. Kwa mujibu wa mkuu wa mkoa serikali pia imetoa Sh bilioni 2.6 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 115 vya madarasa katika shule za sekondari.

Mwenyekiti mpya wa CCM Mkoa wa Songwe, Radwell Mwampashe anakiri kuwa viongozi waliomtangulia wamefanyakazi kubwa ya kuirejesha CCM katika nafasi yake. Katika kusherehekea za maadhimisho ya miaka 46 ya Kuzaliwa kwa CCM, mwenyekiti huyo wa CCM aliwakabidhi vyeti na tuzo baadhi ya viongozi kwa kuthamini mchango wao nzuri wa kukijenga chama.

Mwampashe anaahidi ushirikiana na kuendeleza mambo yote mazuri yaliyoanzishwa na watangulizi wote.



Mwenyekiti Mstaafu wa CCM wa Wilaya ya Mbozi, Kapteni Mstaafu Simon Mboya.



Wanachama wa CCM wakiwa kwenye mkutano.

Siasa

# Rais Samia ameonyesha ukomavu, kazi kwenu wapinzani jengeni hoja


Rais Samia Suluhu

Na Dk. Felician Kilahama

ULINGO wa kisiasa hapa nchini, hivi karibuni umefanyiwa mabadiliko yanayoashiria siyo tu ukomavu, lakini pia utashi na dhamira ya kweli ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, katika kuimarisha demokrasia kwa ustawi wa Watanzania wote.

Mabadiliko hayo ni pamoja na yanayoviruhusu vyama vyote vya siasa kuendesha mikutano ya hadhara ili pamoja na mambo mengine, kunadi sera zao kwa wananchi.

Kwa hatua hiyo, nchi imeondokana na zuio lililokuwa linavizuia vyama vya siasa kuendesha mikutano ya namna hiyo licha ya kwamba kisheria ilikuwa inaviruhusu.

Pamoja na kusaidia uhai wa vyama vya upinzani, lakini hatua hii pia ni ya msingi sana kwa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kama chama kinachotawala, maana inatoa fursa kwa vyama hivyo vingine vya siasa, kuendeleza jukumu la kuiamsha pale inaposinzia katika kutekeleza majukumu yake ya msingi.

Vyama vya upinzani sasa vitumie fursa hii kujenga hoja zitakazoisaidia serikali inayoongozwa na CCM kutekeleza kwa haraka sera zake za maendeleo kwa

> **Tukijitathmini tulikotoka, tulipo na tunakoelekea, naweza kusema kwa kiasi fulani tumethubutu, lakini kazi bado kubwa.**




za

wananchi badala ya kuwa vyama vya kulaumu na kulalamika tu.

Itakapofika mwaka 2025, CCM itakuwa ina umri wa takriban miaka 48, umri ambao si mdogo. Baadhi ya Watanzania waliozaliwa wakati huo, hivi sasa ni watu wazima na inawezekana wengine ni viongozi ndani ya Chama.

Kwa hiyo ni kipindi kirefu, ingawa si sana, lakini kinatosha kwa chama kujipima na kujitathmini ipasavyo.



Lipumba - CUF



Mbowe - Chadema

Hata hivyo, kazi hii ya kujitathmini, haiwezi kufanywa na chama tawala pekee yake na badala yake, inahitaji pia msukumo wa vyama vingine.

Ni takribani miongo mitatu sasa imepita tangu nchi yetu iingie katika mfumo wa vyama vingi, mengi yamefanyika na bado yanaendelea kufanyika.

Kama nilivyokwishadokeza, sasa ni zaidi ya miaka 60 tangu tupate uhuru, ni kipindi ambacho nchi kama China na nyingine za aina hiyo, sasa ni mataifa yenye nguvu kubwa kiuchumi na tishio duniani.

Historia inaonyesha kuwa wakati tunapata uhuru, hawakuwa na nguvu walizonazo sasa, je; wamefanyaje au ni mbinu gani walizotumia hadi kufikia hapo walipo? Je, ni nguvu ya 'demokrasia' au kuna 'siri' ya mafanikio yao zaidi ya dhana hiyo?

Kwa upande wetu, ndani ya kipindi hicho cha miaka 60, bado tunahangaikia huduma muhimu za kijamii ukiachilia mbali kuhangaikia uchumi wa viwanda.


Wakati tumepata uhuru, tulitangaza vita dhidi ya adui: 'maradhi', 'ujinga' na 'umaskini.'

Hata hivyo, tukasema ili kupambana sawasawa, tunahitaji miundombinu imara ya barabara na kuwa na vyanzo vya uhakika vya nishati na kuendeleza kilimo chetu ili tupate uhakika wa mazao ya chakula na biashara.

Vita vya kuondoa maadui hao watatu, vinapaswa kwenda sambamba na kuongeza nguvu katika huduma maji, elimu na afya. Hivyo kujenga na kuweka miundombinu imara katika sekta hizo hakukwepeki, licha ya kuwepo kwa siasa safi, uongozi bora na rasilimali za kutosha.

Tukijitathmini tulikotoka, tulipo na tunakoelekea, naweza kusema kwa kiasi fulani tumethubutu, lakini kazi bado kubwa.

Kusema kweli, kama siyo vita dhidi ya 'Nduli hayati Iddi Amini wa Uganda' iliyolisababisha taifa ulazima wa kutumia kwa wingi rasilimali-fedha, vifaa na nguvukazi kubwa bila kutarajia, pengine tungekuwa tumefanya mengi zaidi.



Rungwe- CHAUMA



Zitto Kabwe - ACT

Katika miaka ya 1970, tulikuwa tujenge Bwawa- kubwa la kuzalisha umeme katika eneo la 'Stigler's Gorge', katika Mto Rufiji. Hata hivyo, kwa sababu ya athari za kivita katika uchumi wetu, ikawa imeshindikana.

Hata hivyo, baada ya vita Tanzania ilielekeza nguvu zake katika 'ukombozi wa mataifa' mengine ya Afrika yaliyokuwa chini ya tawala za 'kibeberu.'

Kwa hali hiyo tukawa tumepungukiwa na uwezo wa kushughulikia masuala ya ndani ya nchi yetu yakiwemo ya kupambana na maadui waliokuwa wametangazwa rasmi kitaifa.

Kiuhalisia, huduma za kijamii na masuala ya kiuchumi, bado ni mahangaiko makubwa.

Kwa mtazamo huo, chama tawala na vyama pinzani kwa pamoja, vinapaswa kuwa na mtazamo wa kuiwezesha Tanzania kufikia malengo muhimu ya kuwaletea maendeleo-endelevu Watanzania wote kwa haraka.

Malumbano ya kisiasa na kisera, yalenge katika kuinua hali za maisha ya Watanzania wote na isiwe kuwaneemesha watu wachache tu.

Vyama pinzani visiwe na mtazamo wa kulaumu na kulalamika tu, bali vije na 'hoja za msingi' kuhusu nini kifanyike kwa lengo la kutumia rasilimali nchini kwa faida ya wananchi wote.

Elimu

# Idadi ya wanaokatisha masomo Sekondari za Ruangwa inatisha

**Na Abdul Mitumba, Ruangwa**

WAKATI idadi ya shule za sekondari zinazojengwa wilayani Ruangwa ikiangozeka kutoka mbili mwaka 2007 hadi kufikia 24 mwaka huu, idadi ya wanafunzi wanaoshindwa kuhitimu kidato cha nne nayo pia imeongezeka kwa kasi.

Hadi kufikia mwishoni mwa mwaka jana, wanafunzi 224 kati ya 522 kutoka katika shule sita tu kati ya 12 zilizotembelewa, wameacha masomo. Wanafunzi hao walianza kidato cha kwanza kati ya mwaka 2019 na 2020.

Idadi hiyo ya wanafunzi waliocha masomo ni zaidi ya asilimia 47 na imeanza kutia shaka kwamba, huenda hakuna sababu ya serikali na jamii kuwekeza nguvu kubwa katika ujenzi wa shule na kuimarisha miundombinu yake.

Wakati mwingine unaweza kudhani kuwa, jamii ya watu wa Ruangwa inaichukulia hali hiyo kama jambo la kawaida, hivyo hakuna sababu ya kufanya mipango ya wazi itakayosaidia kuibua sababu za wanafunzi kukatisha masomo na kuchukua hatua ya stahiki.

Uchunguzi uliofanywa kwa miezi kadhaa na mwandishi wa makala haya, umebaini kuwa tangu mwaka 2019, idadi ya wanafunzi wanaokatisha masomo imekuwa ikiongezeka taratibu kila mwaka na sasa inakaribia nusu.

Mwandishi wa makala haya, amekuwa akifuatilia maendeleo ya wanafunzi hao na hali ya ufaulu kwa karibu katika shule 12 za Wilaya ya Ruangwa na sita kati ya hizo zimetoa jibu la kuwepo kwa changamoto hiyo. Baadhi ya shule za sekondari zilizofikiwa ni pamoja na Makanjiro, Nkowe, Nambiranje, Narungombe, Lucas Maria na Luchelegwa ambazo kwa mara ya kwanza mwaka huu, zitatoa wahitimu wa kidato cha nne.

Wakuu wa shule na wenyeviti wa bodi za shule hizo kwa nyakati tofauti, wamekiri kuwepo kwa utoro wa rejareja na wakudumu na kusababisha wanafunzi wengi kuacha masomo.

Hakuna sababu ya moja kwa moja iliyotolewa kuhusu kinachochangia wanafunzi wengi kukatisha masomo, ingawa baadhi ya wazazi na walezi wamedai kuwa kushindwa kufuatilia maendeleo ya kila siku ya wanafunzi ni moja ya sababu.

Mwenyekiti wa Bodi ya Shule ya Sekondari Nkowe, Amina Nnunduma, amesema kupitia risala yake katika mahafali ya kidato cha nne ya shule hiyo kuwa, shule yake imeathirika mno na utoro.

Kupitia risala hiyo, Nnunduma amesema mwaka jana (2022), ni wanafunzi 53 tu kati ya 132 walioanza kidato cha kwanza mwaka 2019, ndiyo waliohitimu kidato cha nne.

"Kwa masikitiko makubwa, vijana wangu (wanafunzi), 79 waliishia njiani na hakuna anayejua kwa sasa wapo wapi na wanafanya nini," amesema. Takwimu hizi hazikumfurahisha hata kidogo Mkuu ya Idara ya Tathmini na Ufuatiliaji wa Asasi ya Kuunganisha Vijana Kimaendeleo Ruangwa (AKUVIKIRU), Bahati Mtapa, ambaye wakati wa mahafali ya shule hiyo mwaka jana, alikuwa mgeni rasmi.

Mtapa ambaye shirika lake limekuwa likitekeleza mradi wa Kuhamasisha Maboresho ya Elimu ya Sekondari katika shule za Wilaya ya Ruangwa, amesema inaumiza mno kuona watoto wengi wanasajiliwa kuanza elimu ya sekondari, lakini wanaomaliza ni wachache.

"Mkuu wa Shule ya Sekondari Likunja, Grace Mallya, amesema mwaka 2019, shule yake ilipokea wanafunzi 99, lakini waliomaliza kidato cha nne mwaka jana ni 54 tu.

"Ukiangalia ni takribani wanafunzi 45 wameishia njiani, jambo ambalo uongozi wa shule haujalipokea vizuri na hatua mbalimbali zimeanza kuchukuliwa ili kukabiliana nalo," anasema.

Changamoto kama hiyo pia imezikumba shule kadhaa ikiwemo ya wasichana ya Lucas Maria ambayo mwaka 2020, iliandikisha wanafunzi 77 wa kidato cha kwanza, lakini hadi kufikia 2022 ilipoingia kidato cha tatu, wanafunzi 15 wameishia njiani na kusaliwa na wasichana 62 tu. Shule nyingine iliyofikiwa na kukutwa na changamoto za wanafunzi kukatisha masomo ni Makanjiro, ambayo mwaka 2019, iliandikisha wanafunzi 72, lakini hadi 2022 ilibakiwa na 36.

"Ukiangalia hapo ni sawa na nusu kwa nusu waliokatisha masomo na waliomaliza.

Ni takwimu mbaya zisizofaa kuonekana zikiendelea kuonekana katika miaka ijayo," alisema Mjumbe mmoja wa bodi ya sekondari aliyeomba jina lake lihifadhiwe.

Shule hizo sita ni kati ya 12 zilizofikiwa na Mradi wa Kuhamasisha Maboresho ya Elimu ya Sekondari wilayani Ruangwa ulioanza mwaka 2017 na kuratibiwa na AKUVIKIRU.


Nyingine ni Luchelegwa Sekondari, Hawa Mchopa, Kassim Majaliwa, Chunyu, Narungombe, Mandarawe, Matambarale, Namichinga, Chibura na Ruangwa High School. Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa, Andrew Chikongwe, anasema pamoja na changamoto ya utoro, wilaya yake imefanikiwa kujenga shule nyingi katika kipindi kifupi na kwamba hiyo imetokana na wananchi kuamua kujitolea kujenga shule hizo katika hatua za awali na serikali kumalizia majengo. Anasema utaratibu huo umesaidia sana kupatikana kwa shule hizo na kuvuka lengo la Sera ya Elimu, inayoelekeza kila kata iwe na shule moja ya sekondari,huku Kata za Narungombe, Mnacho na Nachingwea, kila moja ikiwa na shule mbili. "Mfano, Kata ya Narungombe ina sekondari mbili za Liunguru Girls na Narungombe Boys. Kata ya Mnacho ina Mnacho Sekondari na Lucas Maria wakati Shule za Ruangwa Girls High School na Kassim Majaliwa, zinapatikana katika kata ya Nachingwea, " amesema Chokongwe.

Ofisa Elimu Sekondari wa Wilaya ya Ruangwa, Ernest Haule, amesema Kata za Mbwemkuru na Nanganga ambazo awali hazikuwa na shule za sekondari, sasa zimepata shule na tayari mwaka huu zimeanza kupokea wanafunzi.

**Muhtasari wa shule na idadi ya wanafunzi walioanza kidato cha kwanza na kukatisha masomo;-**

| Na. | Jina la shule | Walioanza kidato cha 1 kwa 2019 | Walioacha masomo | Waliomaliza kidato cha IV |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Nkowe High School | 132 | 79 | 53 |
| 2. | Likunja Sec School | 99 | 45 | 54 |
| 3. | Mandawa Sec School | 75 | 20 | 55 |
| 4. | Makanjiro Sec School | 69 | 31 | 38 |
| 5. | Lucas Maria Sec School | 77 | 15 | 62 |
| 6. | Luchelegwa Sec School | 70 | 34 | 36 |
| | **JUMLA** | **522** | **224** | **298** |

**Kwa masikitiko makubwa, vijana wangu (wanafunzi), 79 waliishia njiani na hakuna anayejua kwa sasa wapo wapi na wanafanya nini**






## Elimu

# ... Kibiti yaweka mikakati kukabili mimba, utoro na ufaulu hafifu

**Na Mwandishi Wetu, Kibiti**

NI malengo ya kila mzazi/mlezi anapompeleka mwanawe shule afaulu, afanye vizuri ili baadaye apate kujitegemea, kujiajiri au kuajiriwa na kusaidia familia, jamii inayomzunguka na Taifa kwa ujumla.

Pale inapotokea kuwa na ufaulu duni, mzazi mwenye mwamko wa elimu, anakuwa mfuatiliaji kwa walimu na kutenga muda wa ziada kumfuatilia mwanawe kutatua vikwazo vinavyomrudisha nyuma kwenye masomo yake.

Si matarajio ya wengi kusomesha watoto wao kisha wawe wazururaji mtaani na kufanya mambo mengine ya kuichukiza familia yake na jamii kwa ujumla.

Ni kwa mantiki hiyo, ndipo viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti baada ya kuona ufaulu wa wanafunzi unashuka, walipoamua kukutana ili kuweka maazimio ya namna ya kukabiliana na changamoto hiyo.

Kibiti ni moja ya Halmashauri tisa za Mkoa wa Pwani na ni eneo ambalo jitihada za dhati zinatakiwa katika kuweka mikakati ya kuinua kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari.

Kikao cha wadau wa elimu kilichofanyika hivi karibuni katika Shule ya Sekondari Kibiti, pamoja na mambo mengine, kilijadili namna ya kukabiliana na mimba za ututoni, utoro na suala la wanafunzi kujishughulisha na biashara wakati wa masomo.

Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Kibiti, Meja Edward Gowele, aliyekuwa Mwenyekiti wa kikao hicho, anaeleza kuwa msingi wa maendeleo sehemu yoyote ni elimu.

Meja Gowele anasema kiwango hafifu cha ufaulu kwenye mitihani ya kitaifa, kinasababisha kuwa na maendeleo madogo ya kitaaluma.

Anasema Kibiti inahitaji mabadiliko kuanzia kwa wazazi ambao watasaidia kuwafuatilia kwa karibu watoto wao na kudhibiti utoro unaosababisha wasifanye vizuri darasani.

Akiwa katika kikao hicho, Meja Gowele anawasisitiza wazazi kujenga ushirikiano na walimu na kuwachukulia hatua watoto wanaokutwa kwenye maeneo ya biashara muda wa masomo.

"Tushirikiane kuwachukulia hatua tunapoona mtoto anafanya biashara kipindi cha masomo, hata kama siyo mwanao, chukua hatua na mzazi wake akikujia juu, tupate hizo taarifa, bila kufanya hivi, elimu Kibiti itaendelea kushuka." anasema.

Aidha, anaeleza kuwa ili kudhibiti ongezeko la mimba shuleni, ni vema wazazi kutoa ushirikiano kwa wale wanaowaoa na kuwapa mimba wanafunzi.

Aidha, Meja Gowele anawashauri viongozi wa dini kuzungumzia suala la elimu wakiwa kwenye nyumba za ibada akisema kwa kufanya hivyo, kutaleta tija.

Kadhalika, anaelezea umuhimu kwa wazazi kuchangia chakula shuleni ili wanafunzi wasome kwa bidii badala ya ilivyo sasa kwa shule nyingi ambazo hazina utaratibu huo.




"Tuweke kiasi cha fedha kwa ajili ya kuchangia chakula cha watoto wetu wanapokuwa shuleni pamoja na mahitaji mengine ya shule," anasisitiza.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti, Mohamed Mavura, anaeleza kuwa kikao cha wadau wa elimu kimekuwa kikifanyika kila mwaka, lakini bado kuna mambo yanawarudisha nyuma.

Mavura anasema katika kikao cha mwaka huu, wamejikita zaidi kwenye vikwazo vya ufaulu, kujiuliza na kujadili kwanini vinaendelea na nini kifanyike kuviondoa.

Anasema serikali inatoa fedha nyingi katika sekta ya elimu, hivyo ni jukumu la jamii kuungana kuondoa vikwazo na kupambania ufaulu wa wanafunzi ngazi ya msingi na sekondari.

"Tujifikirie zaidi kuendeleza elimu hapa Kibiti kwa kuwashirikisha wadau, ushirikishwaji ni muhimu kwenye maendeleo ya elimu, nataka niache alama katika sekta hii, ufaulu uongezeke na kila mzazi aone umuhimu wa elimu kwa kumsomesha mtoto wake," anasema Mavura.

**Tukijitathmini tulikotoka, tulipo na tunakoelekea, naweza kusema kwa kiasi fulani tumethubutu, lakini kazi bado kubwa.**

Aidha, anasema wapo baadhi ya wazazi wanaotakiwa kubadilika kwani wakati mwingine serikali inatumia nguvu kuwarudisha wanafunzi shuleni, lakini baada ya muda wanaonekana mitaani kwenye sehemu za biashara muda wa masomo, hali hiyo ni kuendelea kuidumaza elimu.

" Tunatumia nguvu kumrejesha mwanafunzi shule, lakini baada ya siku chache, wanarudi kuendelea na biashara, wakikamatwa wazazi ndiyo wanaandamana kwenda kwa Mkuu wa Wilaya kuomba watoto waachiwe huru watarudi shule, lakini wanarudi tena kule walikotolewa. Hii haituvushi, tunatakiwa kubadilika," anasema.

Ili kukabiliana na njaa kwa wanafunzi, Mavura anashauri kila shule kutumia maeneo waliyonayo kupanda mihogo na mazao mengine ambayo yatatumika kama chakula kwa wanafunzi.

" Watoto wanatembea umbali mrefu, wakifika shule hakuna chakula, kwa hali hii hawawezi kufanya vizuri kwenye mitihani yao, tubadilike tuipe elimu kipaumbele, tuungane kukabiliana na njaa kwa watoto wetu wanapokuwa shuleni," anasema Mavura.

Afisa Elimu Sekondari, Anna Shitindi, anasema bado kuna kikwazo cha elimu kwa baadhi ya wazazi na walezi kuwashawishi wanafunzi kufanya vibaya kwenye mitihani yao ya shule ya msingi kwa lengo la kukwepa majukumu ya kuwasomesha.

Kukosekana kwa chakula cha mchana, ujauzito na upungufu wa miundombinu, pia vinatajwa kuchangia kushuka kwa ufaulu,

"Tamaduni zilizopitwa na wakati, kukithiri kwa utoro kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari pamoja na ushirikiano hafifu kutoka kwa wazazi katika kusimamia maendeleo ya kitaaluma, pia ni vikwazo vya ufaulu," anasema.

Hata hivyo, Shitindi anasema ipo mikakati ya kukabiliana na vikwazo vya elimu ambayo ni pamoja na kuielimisha jamii umuhimu wa elimu na kuelewa kuwa elimu ni haki ya msingi kwa kila mtoto.

Anaeleza kuwa mikakati mingine ni pamoja na kuihamasisha jamii kujitoa katika ujenzi wa miundombinu mbalimbali kulingana na vipaumbele.

"Katika mikakati yetu, pia tumeweka suala la kuhamasisha jamii kuhusiana na umuhimu wa kuchangia chakula ili wanafunzi wapate chakula cha mchana, lakini pia kuhamasisha shule kulima mbogamboga kwa ajili ya matumizi ya wanafunzi," anabainisha.

Aidha, anasema idara hiyo inawaomba wadau wa elimu kushirikiana katika kudhibiti utoro wa wanafunzi na kutoa elimu kwa jamii kuhusiana na tamaduni zilizopitwa na wakati.

Hamidu Ungando, Diwani wa Kibiti anasema sababu zinazochangia ufaulu duni kwenye shule zilizopo katika kata yake ni pamoja na msongamano wa wanafunzi katika darasa moja.

"Mfano katika Shule ya Sekondari Zimbwini, wanafunzi wapo 2,400, katika matokeo ya kidato cha pili, waliofanya mtihani walikuwa 629, waliofeli ni 243 yaani wote wamepata divisheni sifuri, daraja la kwanza wawili, daraja la pili wanne, daraja la tatu 20 na la nne 256," anabainisha.

Anasema hali hiyo pia ilichangiwa na baadhi ya wanafunzi kutembea umbali mrefu na wakifika shuleni, wamechoka huku kukiwa hakuna huduma ya chakula shuleni.

"Mtoto anasoma mbali na anapooshi, akifika shuleni anakuwa amechoka na hakuna chakula, hii imechangia baadhi ya watoto wa kike kujiingiza kwenye tamaa na kukubali lifti ambazo zimewagharimu baadhi yao kupata mimba na kushindwa kuendelea na masomo," anasema na kuongeza:-

"Kwa mwaka jana katika kata yangu, wanafunzi wa kike 18 walikatisha masomo kutokna na ujauzito na watuhumiwa wengi wa mimba hizo wanadaiwa kuwa ni madereva wa bodaboda ambao huwapa `lift' kutokana na hali za wazazi wao kuwa duni na kushindwa kuhimili mahitaji ya nauli," anaeleza Ungando.


Ungando pia anaeleza kuwa mwamko wa elimu kwa baadhi ya wazazi, ni kikwazo kwani baadhi yao hawafuatilii maendeleo ya watoto wao kwa walimu na hata wanapoitwa kwenye vikao, hawaendi.

"Mfano ni hiyo shule, ina wanafunzi zaidi ya 2,000 kikiitishwa kikao wanaweza wakafika wazazi 200, kwa hiyo hata utekelezaji wa maazimio haufanyiki kama inavyotakiwa, lakini pia hata wakitakiwa kulipa Sh. 1,000 kwa wiki ili mtoto apate angalau uji kwa siku akiwa shuleni, nayo hawatoi kama inavyotakiwa na hivyo kumfanya mtoto asome akiwa na njaa," anasema.

Anaeleza kuwa jitihada zinaendelea kukabiliana na vikwazo hivyo ikiwa ni pamoja na kuendelea kuwaelimisha wazazi kuipa kipaumbele elimu.

Siasa

# Kujisahihisha kwa kiongozi si kujidhalilisha



RAIS wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere, wakati wa uhai wake, aliandika vitabu kadhaa vilivyolenga pamoja na mambo mengine, kuuelimisha umma masuala mbalimbali ya kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Moja ya vitabu hivyo, ni `TUJISAHIHISHE.' Kitabu hiki kimekuwa kikitumika na baadhi ya viongozi wa chama na serikali kama nukuu/rejea katika hotuba zao mbalimbali.

Makala hii inakiangalia kitabu hiki undani wa maudhui yake na shabaha ya mtunzi, Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Nyerere.

Mwalimu Nyerere aliamini kuwa hakuna binadamu awe kiongozi au asiye na nafasi yoyote ya uongozi katika jamii, aliyekamilika kwa asilimia zote, hivyo kukosea, ni jambo la kawaida.

Lakini, pamoja na kwamba kukosea kwa binadamu ni jambo la kawaida, Mwalimu Nyerere aliona umuhimu wa kujikosoa ama kujisahihisha.

Watu wengi hususan viongozi, hujihisi kuwa wanapojisahihisha wakati wanapofanya makosa ni ama udhaifu au kujifedhehesha kwa wanaowaongoza.

Lakini, ukweli ni kwamba, kujisahihisha, ni nguzo muhimu katika uongozi.

Hayati Mwalimu Nyerere akiwa kiongozi mkuu wa chama na serikali wakati huo, kupitia katika kitabu chake cha TUJISAHIHISHE, alilenga katika kuwahimiza viongozi wenzake, kuepuka makosa na wanapokosea, wawe na ujasiri wa kujisahihisha japo kujihukumu mwenyewe ni jambo gumu.

"Nimejaribu kueleza makosa machache ambayo yafaa tuyaondoe na kuyaepuka katika chama chetu. Sitaki mtu yeyote afikiri kuwa mimi niliyeandika maneno hayo, sina makosa. Hivyo, si kweli," Mwalimu Nyerere alisisitiza katika kitabu chake hicho cha 'TUJISAHIHISHE.'

Katika kitabu hicho, Mwalimu anaeleza kuwa, Chama (TANU) wakati huo, hakikuundwa kwa faida ya mtu au kikundi wala kutoa tuzo, iwe kwa kiongozi ama kwa mwanachama, na haikumuahidi mtu yeyote mshiriki katika Chama kwa hulka ya ubinafsi, kuwa chama kitamfanyia jambo fulani kama tuzo.

"Kujikuhumu ndani ya chama na utumishi wa umma, itatusaidia siyo tu katika kuwahukumu wenzetu jambo ambalo ni rahisi, lakini pia katika kujihukumu sisi wenyewe, ambalo ni jambo gumu na la maana zaidi," anasema Mwalimu Nyerere katika kitabu hicho.

Mwalimu anaendelea kufafanua kuwa, matatizo mengi ya wanadamu yanatokana na ubinafsi ambao ni wa aina nyingi na kuwataka viongozi katika ngazi zote za chama na serikali kujifunza kusikilizana na kuzijibu kwa kuzikubali au kuzikataa hoja wanazoziibua na kuzisema kwa wananchi.

"Tujifunze kusikiliza hoja zenyewe zinazotolewa na wenzetu na kuzijibu kwa kuzikubali au kuzikataa, bila kujali kama aliyezitoa ni rafiki au si rafiki. Pia, wanaopingwa hawana budi kukubali kuwa kinachopingwa ni hoja zao, siyo wao," anafafanua.

Aidha, anasema "ukweli una tabia moja nzuri sana; haujali mkubwa wala mdogo; haujali adui wala rafiki. Ukweli haupendi kupuuzwa puuzwa."

Katika kusisitiza kauli yake hiyo, aliwataka viongozi kuuelewa umuhimu wa kujielimisha bila kikomo kwa sababu kujielimisha ni kutafuta ukweli wa mambo.

"Ni wajibu wetu kujitahidi kadiri iwezekanavyo kuzipa akili zetu uhuru wa kufanya kazi bila kutu na uchafu wa aina nilioutaja," Mwalimu Nyerere anaasa na kuongeza:

"Kadhalika, hoja zetu zikijibiwa kwa kupingwa halafu tunawakasirikia waliozipinga, tunafanya mazungumzo yasiwe na maana, kwa sababu tunapenda hoja zetu zikubaliwe tu hata kama si safi."

"Watu walio hatari sana ni wale ambao wanafikiri kuwa wanajua kila kitu, wala hawana haja ya kujifunza zaidi. Hii ni tabia mbaya ambayo huzuia kabisa maendeleo. Sababu moja ambayo ilituzuia sisi Waafrika kuendelea ni majibu ya urahisi kwa matatizo makubwa. Shamba letu kama halikutoa mavuno ya kutosha, jibu lilikuwa wazi; au limerogwa au ni amri ya Mungu."

Kosa lingine, linalofanywa na baadhi ya viongozi ni kuyafanya mawazo na matakwa ya nafsi zao kuwa ni mawazo na matakwa ya raia.

"TANU ilianzishwa na iliundwa kujishughulisha na haja za Jumuiya kwa ujumla. Anayefikiri iliundwa kwa faida yake binafsi na kwamba ilipoundwa ilimuahidi kwamba ikiwa atakubali kuwa mwanachama au kiongozi, basi itamfanyia jambo fulani kama tuzo, anakosea!" alisisitiza.

Kwa mujibu wa maandiko ya kitabu chake hicho, kosa lingine kubwa kwa baadhi ya viongozi ni kuwagawa watu katika makundi, kundi "letu" na kundi "lao." Wakati mwingine "sisi" ni viongozi tunaochaguliwa kwa kura za wanachama. Hili ndilo kundi "letu." Viongozi wengine ni wale wanoajiriwa. Baadhi ya viongozi wanochaguliwa hujiona kuwa ni mabwana na kwamba viongozi wanaoajiriwa ni watumishi tu ambao hawastahili kuheshimiwa.

Mwalimu anazidi kusisitiza katika kitabu chake kwamba "Kama wanachama wa TANU na hasa viongozi, hawatakihukumu Chama chetu kwa mahitaji ya Jumuiya, bali watakihukumu kwa mahitaji ya nafsi zao wenyewe, chama hakitadumu. wanachama wa aina hiyo ni ugonjwa katika chama."

"Ni dhahiri kwamba yule asiyetambua ubora wa elimu na ujuzi, ni mjinga ambaye Chama hakina budi kumsaidia kwa kumuondolea adui huyo anayemsumbua, yaani ujinga" anasema Mwalimu Nyerere katika kitabu hicho na kufafanua.

"Kujielimisha ni kutafuta ukweli wa mambo. Elimu ya kweli ni ujuzi wa sababu za mambo mbalimbali, na kama ni mambo mabaya, ni kujua jinsi ya kuyaondoa; na kama ni mema, jinsi ya kuyadumisha."

Anasema: "Mpumbavu ni yule anayeyapa mambo sababu zisizo za kweli na kushauri dawa isiyo ya kweli katika kutafuta sababu za matatizo, na jinsi ya kuyaondoa. Kila mmoja wetu anacho chombo cha kutumia akili yake. Jambo la maana ni kuzipa akili uhuru kamili kutafuta elimu bila kutiwa kiinimacho na utashi wetu wa unafsi."

Dalili nyingine ya ubinafsi, anaeleza kuwa ni ugonjwa mbaya sana ni fitina. Kanuni moja ya TANU inasema 'Nitasema kweli daima fitina kwangu ni mwiko.'

"Lakini bado tunao wanachama ambao ni wafitini wakubwa bila kujitambua. Ni wa aina mbalimbali. Wengine humuona mwenzao anafanya kosa. Badala ya kumwambia palepale kijamaa kwamba atendalo ni kosa, watanyamaza kimya. Lakini hawanyamazi kabisa! Watakwenda kumteta katika vikundi vya siri. Matendo haya si ya kumsaidia mwenzao, ni ya kumdhuru."

"Makosa yetu megine hutokana na woga, woga unaotuzuia kumlaumu mkubwa japo tunajua kuwa kakosa, au kumtetea mdogo anayelaumiwa na wakubwa japo tunajua kuwa hana makosa. Na msingi wa woga pia, ni unafsi. Pengine huwa tunaogopa sisi wenyewe kulaumiwa au kupata hasara fulani." anafafanua na kuongeza:

Demokrasi inawapa haki, na ukweli unawapa wajibu wa kuendeleza mawazo yao mpaka wengi waone kuwa ni ya kweli. Bila hivyo, maendeleo katika mawazo hayawezekani, kwani mara nyingi wazo zuri hutokana na mtu mmoja tu. Mwanzo laweza likapingwa, pengine kwa nguvu kabisa na walio wengi, lakini hatimaye wengi hulikubali. Huu ndiyo msingi

**Tukijitathmini tulikotoka, tulipo na tunakoelekea, naweza kusema kwa kiasi fulani tumethubutu, lakini kazi bado kubwa.**

# Siri mwajiriwa, mwajiri kugombewa na wengi

**Na Paul Mng'ong'o**



AJIRA ni neno kubwa katika jamii yoyote ile hapa duniani. Ni jambo nyeti sana kwa sababu linabeba maana kubwa ya uchumi wa nchi yoyote na watu wake.

Historia inatueleza kwamba, awali hakukuwa na neno ajira, badala yake kulikuwa na neno `kazi.'

Hata hivyo, kazi ilianza tangu kuumbwa kwa misingi ya dunia au tangu mwanzo wa mwanadamu na ilifanyika kwa manufaa ya mtu binafsi na kuchagiza manufaa ya familia, ukoo na jamii kwa jumla.

Kazi ilifanyika ili kutosheleza mahitaji ya msingi ya mwanadamu ambayo ni chakula, malazi na makazi.

Mtu alilazimika kufanya kazi kama uwindaji kwa ajili yake na familia, lengo likiwa ni kumwezesha kupata chakula na mavazi ya ngozi. Na hata baadhi ya vitabu vitakatifu vinasisitiza `Asiyefanya kazi na asile.'

Lakini pia mtu alikata miti na kujenga mahali pa kuishi, kupata kuni nakadhalika. Maisha yalitegemea sana matunda pori na nyama kama chakula.

Maisha yalikuwa huru na rahisi, hakukuwa na mtu mmoja kumtumikisha mwingine sababu maisha yalitegemea zaidi asili.

Wakati huo mgawanyo wa kazi ulizingatia umri, jinsia na matabaka

Hata hivyo tafiti zinaonesha kuwa tangu awali mgawanyo wa majukumu katika jamii ulizingatia zaidi umri na jinsia, wakati matabaka yalianza kuchipua baadaye kulipoanza kutokea kwa matumizi ya akili kwenye ubunifu na kukua kwa teknolojia.

Kipindi chote kulikuwa na kazi na wala si ajira, mabadiliko ya hatua yalianza kulingana na ukuaji wa teknolojia, uvumbuzi na ugunduzi ulipoongezeka.

Ukuaji huu ulianza kuleta nyenzo za kufanyia kazi na baadaye zaidi, kuanza kuibuka kwa watu waliohitaji watu wenzao kuwafanyia kazi.

Bila kujali ngazi na hatua za ukuaji wa kazi kwa mahitaji ya msingi ya mwanadamu mwenyewe mpaka ajira, ni muhimu kujua kwanza neno ajira linamaanisha nini?

Ajira ni neno la jumla linalo maanisha muunganiko baina ya mwekezaji, kazi husika, mtumishi (mwajiriwa) na malengo yao.

Neno ajira mara nyingi limekosewa sana na pande zote mbili (mwekezaji na mtumishi).

Makosa yanayofanywa na pande hizi mbili kwenye ajira ndiyo sababu ya kutofanikiwa kwa wote, unyonyaji, wizi, kutoendelea kwa biashara na matatizo yote yanayotokea kwenye mahusiano ya ajira.

Makosa tunayoyazungumzia yanaanzia kwenye kiini cha mtazamo wa pande zote mbili.

Mwekezaji anapoanzisha uwekezaji wake, lengo lake kuu ni kupata faida wakati mwajiriwa anapokuja kutafuta kazi anahitaji kupata aina fulani ya utoshelevu kwenye maisha yake.

Mara nyingi uhitaji wa mwajiriwa, huanzia kwenye utoshelevu wa maisha ya kawaida kwa maana ya kuyamudu mahitaji ya lazima ya binadamu kwake yeye na wategemezi wake.

Hiki ndicho kiwango cha chini cha utoshelevu na kinaendelea kupanda kwa kadiri mwajiriwa alivyowekeza kwenye uwezo wake wa kuzalisha thamani. Lengo la makala haya ni kuboresha mtazamo wa kila upande kwa sababu kama mitazamo hiyo ikiwa bora na chanya, kila upande utanufaika na ajira na kufikia lengo.

Tukianza na mwekezaji, yeye anachohitaji ni kupata faida kutoka kwenye uwekezaji wake, faida itakayomwezesha kufurahia maisha na kuwekeza zaidi. Lakini faida hii ataipata kwa kuwa na watu (waajiriwa) ambao watakuwa na uzalendo kwenye kazi yao, wataipenda kazi na kuifanya kwa moyo, kwa juhudi, ubunifu na ubora.

Kutokana na tatizo la kimtazamo, kinachoangaliwa ni faida ya mwisho badala ya kuangalia mazingira yatakayoleta faida ya mwisho.

Hapa ndipo tunasema "watu wengi wenye mafanikio ya kweli kiuchumi, mtazamo wao au nguvu yao kubwa haikuelekezwa kwenye kujipatia fedha."

Wazo la faida pekee bila kuangalia mazingira, linaweza kutoa matokeo makubwa kwa haraka, lakini matokeo hayo huwa hayadumu.

> **Watu wengi wenye mafanikio ya kweli kiuchumi, mtazamo wao au nguvu yao kubwa haikuelekezwa kwenye kujipatia fedha**

Kwa mfano, ili mwekezaji apate mafanikio, hahitaji tu kuwa na mwajiriwa bali anahitaji ubora fulani wa mwajiriwa ambao unapatikana kwa uwezo wake na mazingira ya kazi na hapo mazingira yakiwa na mchango mkubwa.

Makala haya yanatoa rai kwa wawekezaji wote kuhakikisha kuwa wanafanya kila linalowezekana kuipata kwanza saikolojia ya watu wanaowaajiri kwa kuwaandalia mazingira bora ya kazi na maslahi toshelevu ili kuwapa mazingira mazuri ya kutoa kila walichonacho kwa ajili ya kazi yao.

Mwajiriwa anahitaji mambo kadhaa ili aweze kuzalishe kwa kiwango cha juu.

Vitu hivyo ni pamoja na Mazingira bora ya kazi, maslahi toshelevu, mfumo rahisi wa kazi na usimamizi thabiti wenye utu na busara.

Hali kadhalika, usalama kazini, motisha za kifedha na motisha za ndani zisizo za kifedha, kuendelezwa kwa mafunzo, maelekezo na semina za mara kwa mara, vitendea kazi vizuri, kutambulika, kuthaminiwa, kuaminiwa na kushirikishwa.

Mwajiriwa pia anahitaji kupewa mazingira ya usawa yasiyo na chembe ya ubaguzi,

maelewano kazini, mgawanyo mzuri wa kazi, taratibu wazi na zinazoeleweka nakadhalika.

Vitu hivi vinamfanya mfanyakazi kuipenda kazi na kuifanya kwa moyo kwa kuwa kazi yake inakuwa kitu ambacho hawezi kuruhusu kipotee.

Jambo hili likiwepo, huibua ari ya mtumishi kuipenda kazi na kuimiliki na matokeo yake, mwekezaji anapata watumishi waaminifu, wenye juhudi na walio tayari kujitolea kwa ajili ya biashara au kazi yao na hivyo kufanya uzalishaji kuwa mkubwa. Kitendo hicho kinaifanya kazi iwe na matokeo kuwa makubwa na faida kuongezeka.

Kwa msingi huo, unapoanza kuwa mwekezaji na unahitaji kuwa na mtumishi (hata kama ni mmoja), lazima umhakikishie mambo hayo na kumshirikisha kwenye kuyaendea mpaka kuyafikia sababu uwekezaji mwingi hauanzia hatua ya kwanza na utimilivu wa mambo haya yote.

Kwa upande wa pili wa dhana ya ajira, kuna watumishi ambao ndiyo huitwa waajiriwa. Watu hawa pia kwa asilimia kubwa (wengi wao) wamekuwa na dhana au mtazamo usio sawa kwenye ajira.

Wengi wanapofikiria ajira, wanafikiria fedha mwisho wa mwezi. Jambo hili pia limeathiri utendaji wa waajiriwa wengi sana sababu mtazamo upo kwenye kupokea badala ya kuweka mtazamo na nguvu kubwa kwenye thamani na matokeo atakayoyaleta mezani.

Katika sehemu hii, mwandishi wa makala analenga kuuasa upande wa waajiriwa mmoja mmoja, kujenga mtazamo sahihi kuhusu ajira yake kwa sababu hapo ndipo itakapompa matokeo makubwa, yenye amani na ya kudumu.

Kila mwajiriwa akitaka kufanikiwa na kukua, lazima awe na wazo la kiuwekezaji na vivyo hivyo mwekezaji akitaka kufanikiwa, lazima awe na wazo la mtumishi kichwani mwake.

Hii `double entry,' ndiyo huleta mafanikio kwenye ajira kwa pande zote mbili. Hakuna mwajiri (mwekezaji atakayepata mafanikio ya kudumu kama hatajibu maswali na mahitaji ya muhimu ya mwajiriwa.

Na vivyo hivyo, hakuna mwajiriwa atakayepata mafanikio ya kudumu kama hatakuwa na jibu la maswali au mahitaji ya mwekezaji.

Huu ndiyo mtazamo ambao watu wengi wanaukosa katika mambo mbalimbali.

Mafanikio hayawezi kuja kwa kusimamia mtazamo wa kupokea, bali watu watakutafuta popote ulipo kama utatoa jawabu la maswali, mahitaji au changamoto zao. Hivyo mafanikio yanaletwa na mtazamo wa kutoa na siyo kupokea.

Nafasi kubwa ya kufanikiwa kwa mwajiriwa hasa katika dunia ya sasa, ni thamani anayoileta kwenye uwekezaji uliomwajiri.

Mtu unapopata ajira kwa maana kuwa mwajiriwa, ni vizuri ukajipanga kwenye mambo muhimu ambayo wewe utayatoa kama:

Nidhamu kazini kwa maana ya kufuata taratibu na miongozo, kuwa na bidii na kufanya kazi zaidi ya malengo yaliyowekwa ya matokeo na si ukamilifu tu wa kazi (dunia ya sasa mwekezaji akiwakilishwa na menejimenti, wanataka matokeo)

Mwajiriwa pia anapaswa kujitathmini na kutoa ripoti ya kuonyesha kiwango cha juu cha ubunifu kwenye kazi, kuonyesha kiwango cha juu cha ubora, kuwa msaada kwa wengine.

Hali kadhalika mwajiiriwa anapaswa kuwa mshauri na si mkosoaji, apende kujifunza na kufanya kazi kwa wakati bila kupoteza muda.

Haya ndiyo mambo ambayo humpa mwajiriwa kibali na kukubalika sana kwa mwajiri yeyote. Hakuna mwajiri atakayeruhusu kirahisi kumpoteza mtumishi mwenye sifa hizi.

Kwa sifa hizi, mwajiriwa hulindwa, hupewa nafasi za juu zaidi, huongezewa mshahara, huendelezwa na kisha hugombaniwa na waajiri wengine kwa maslahi mapana zaidi.

Maana yake ni kwamba kama unahitaji kupendwa na kupewa nafasi, acha kuja kazini au kwenye ajira na mtazamo wa mshahara tu.

Mwisho makala haya yanasisitiza kuwa, ili kuboresha uwanda wa ajira nchini na kwingineko duniani, ni muhimu kujua kuwa kila upande wa ajira, una mahitaji muhimu na ya msingi yanayosaidia kuhitajiana.

Hivyo lazima kila upande uwe kila upande kujibu maswali ya upande mwingine kwa nguvu zote na kwa utimilifu.

Hili linawezekana kama upande wa waajiriwa wataachana na mtazamo wa kudai na kufikiria kupata tu, bali nguvu kubwa waiweke kwenye kutambua na kujibu mahitaji ya mwekezaji kwa kutoa thamani kuhakikisha kuwa lengo la mwekezaji linatimia kwa asilimia zote.

Kama wataanzisha vikao na vikundi, jambo la msingi liwe kujadili jinsi ya kuongeza thamani kwenye uwekezaji wakijua kuwa kwa azma hiyo watakuwa wanaongeza thamani yao kwa mwekezaji na hakuna mwekezaji atakayetamani kuwapoteza.

Kwa upande mwingine, lazima mwekezaji ahakikishe kuwa mtazamo na nguvu zake zote ni kujibu mahitaji ya waajiriwa wake.

Ni muhimu mwekezaji kuhakikisha kuwa mazingira bora na rafiki ya kazi na maslahi ya kuridhisha huku akitumia zaidi misingi ya utu badala ya sheria pekee na ukandamizaji wa adhabu tu.

Haya yakizingatiwa, hapana shaka mahali pa kazi patakuwa salama.



Kuruti katika jeshi la Ukraine akirusha kombora dhidi ya jeshi la Urusi katika mapigano yaliyofanyika jana mjini Bakhmut, Donetsk (PICHA: Reuters)

# Marekani, Urusi zaihofisha dunia

MATAIFA mawili makubwa na yenye nguvu kubwa kijeshi duniani, yamenuniana.

Hayaaminiani. Ukimya na kurushiana vijembe uliodumu kwa miezi kadhaa sasa kati ya mataifa hayo ya Urusi na Marekani, si ishara njema kwa watu.

Kwenye diplomasia, wanasema wanapopigana "mafahari wawili," zinazoumia ni nyasi. Maisha ya watu yapo kwenye hofu kubwa kama si hatarini.

"Kuaminiana kati ya mataifa haya makubwa duniani hakupo tena," Waziri wa Mambo ya Nje wa China, Wang Yi, alikiri Jumamosi iliyopita akiwa katika mkutano wa 59 kuhusu usalama, uliofanyika Munich.

China ni ya kwanza duniani kwa idadi kubwa ya wanajeshi ikiwa na askari milioni mbili, wakati Marekani ikiwa ya tatu kwa kuwa na wanajeshi milioni 1.39 baada ya India inayoshikilia nafasi ya pili ikiwa ina wanajeshi milioni 1.45.

Hata hivyo, Marekani inashikilia nafasi ya kwanza kwa bajeti kubwa ya kijeshi. Bajeti ya jeshi la nchi hiyo ni Dola bilioni 801 wakati China inashikilia nafasi ya pili kwa kulitengea jeshi lake bajeti ya Dola bilioni 293 za Marekani.

Bajeti ya Jeshi la Urusi ni Dola bilioni 65.9 na kwa mtiririko huo, inashikilia nafasi ya tano. India kwa upande wake, inashikilia nafasi ya tatu kwa bajeti ya Dola bilioni 79.6 na Uingereza ni ya nne kwa bajeti ya Dola bilioni 68.4 za Kimarekani.

Hata hivyo, linapokuja suala la kumiliki silaha za nyuklia, Urusi inashikilia nafasi ya kwanza kwa kuwa na makombora 6,257 ya nyuklia. Mtandao wa Wikipedia unakadiria kuwa Urusi ina vichwa 5,550 vya makombora ya nyuklia makadirio ambayo ni ya chini kabisa kuliko uhalisia.

Marekani inashikilia nafasi ya pili kwa kuwa na vichwa 5,550 vya makombora ya nyuklia na China ni ya tatu ikiwa na vichwa 350 vya nyuklia.

Marekani ni nchi pekee duniani iliyowahi kutumia makombora yake ya nyuklia mara mbili katika vita vya Hiroshima na Nagasaki, huko Japan, nchi ambayo sasa inatazamwa kama mshirika wa Marekani kijeshi.


Katika vita vya Ukraine ambavyo Februari 24, mwaka huu itatimiza mwaka mmoja, Marekani inahofia kuwa Urusi itaungana na China kijeshi. Kama kweli nchi hizi mbili washirika zitaungana, zitakuwa na jumla ya mambora 6,607 ikilinganishwa na makombora 5,550 ya Marekani. Kwa maneno mengine, Marekani itakuwa inazidiwa makombora 1,057 (sawa na asilimia 19).

Katika mkutano wa wiki iliyopita kuhusu usalama, China ilituhumiwa kwa kutaka kula njama na Urusi, kama njia ya kukabiliana na nchi za Umoja wa Ulaya na Marekani katika vita vya Ukraine.

Hata hivyo, Waziri Wang Yi wa China, alidokeza kwamba hivi karibuni Rais Xi Jinping atawasilisha pendekezo la mpango wa amani, wenye lengo la kumaliza kile mamlaka ya China inachokiita kuwa ni mgogoro na si vita huko Ukraine.



Rais wa Marekani, Joe Biden



Rais wa Urusi, Vladimir Putin

Waziri huyo aliwataka wasikilizaji kuamini kauli hiyo na kupuuza madai ya Marekani.

"Tunahitaji kufikiria kwa makini na hasa ninyi marafiki zetu wa Ulaya, kuhusu hatua gani zichukuliwe ili kuepusha kutokea kwa vita. Utaratibu gani ufuatwe ili kuleta amani ya kweli huku Ulaya," alinena waziri huyo.

Mwadiplomasia huyo mwandamizi wa China alipuuza kile alichokiita kuwa majibu ya woga yaliyotolewa na Marekani kuhusu ndege za upelelezi ya China zilizodunguliwa mwishoni mwa Januari na mapema Februari.

"Baadhi ya nchi hazitaki kuona mazungumzo ya amani yanafanikiwa, Hawajali maisha ya Waukraine wanaopoteza maisha yao wala athari wanazozipata watu wa Ulaya. Nadhani wana mipango yao mahususi kuliko Ukraine, vita hivi lazima vikome." alisema Wang Yi.

Usiku wa Jumamosi iliyopita mjini Munich, Waziri Wang na Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Anthony Blinken, walikutana kwa mazungumzo yasiyo rasmi pembezoni mwa mkutano kuhusu usalama.

Wanadiplomasia hao walishtumiana kuhusu mambo mbalimbali. Hata hivyo, Wang hakuomba radhi kuhusu ndege za upelelezi zisizokuwa na rubani, zilivyoingia katika anga la Marekani. Badala yake, Wangf aliishtumu Marekani kwa kutumia nguvu kama jibu kwa China kuhusu ndege hizo.

**Baadhi ya nchi hazitaki kuona mazungumzo ya amani yanafanikiwa, Hawajali maisha ya Waukraine wanaopoteza maisha yao wala athari wanazozipata watu wa Ulaya...**

Kwa upande wake, Blinken alimwambia Wang kuwa China ina mpango wa kuisaidia Urusi katika vita vyake huko Ukraine

Kabla ya Urusi kuivamia Ukraine, Februari 24, mwaka huu, Rais Xi Jinping wa China na Vladimir Putin, waliapa rasmi kwa maneno 5,000 kuhusu ushirikiano usiokuwa na shaka. Mwezi mmoja baadaye, Urusi iliomba rasmi msaada kutoka China ili kukabiliana vema na Ukraine.

"Kwa hiyo sasa tuna adui mmoja, Marekani" kilisema chanzo kimoja.

Katika hali ilivyo sasa, Marekani inaamini kuwa wakati wowote kuanzia sasa China itaivamia Taiwan.

Jenerali mmoja wa jeshi la Marekani aliwahi kutoa tuhuma hizo ambazo wataalam wa vita hawazichukulii kama ni jambo la uongo.

# Hasara isiwavunje moyo wajasiriamali

Na PAUL MNG'ONG'O

MAFANIKIO makubwa huja kwa kuchapa kazi kwa bidii na wengi waliofanikiwa, walizingatia hilo.

Familia nyingi za wafanyabiashara, zinapambana kwa bidii ili kufikia malengo ya kujikimu na kiuchumi.

Hata hivyo ili hayo yaweze kufikiwa, suala la nidhamu lazima lipewe umuhimu katika kuendesha biashara zao,

Wafanyabiashara wengi wanafeli katika kipengele cha kuzingatia muda, jambo ambalo hujikuta wakipata hasara katika biashara zao.

Kwa mazingira ya biashara, ni kawaida kutokea kwa hasara husasan zinazoanza.

Hasara katika biashara, huonekana zaidi pale fedha nyingi zinapopotea kuliko zinapoingia, kwa hiyo lazima kuwe na umakini ili kuepukana na tatizo hilo.

Mtiririko wa hasara huwa katika namna ndogo ikiwemo kukosa jambo muhimu ulilokuwa unalifuatilia, kukosa maarifa ya kuendesha biashara, kupoteza wateja na vifaa vya kufanyia kazi na kubwa zaidi ni kushindwa kulipa mahitaji ya biashara kama vile bili za umeme, mishahara ya wafanyakazi, gharama za mawasiliano na nyinginezo.

Katika hali ya kawaida, si rahisi kumtambua mfanyabiashara au mjasiriamali kupitia hasara anazozipata katika biashara yake, bali ule uwezo wa kupambana na mazingira yanayoleta hasara mpaka kuhakikisha anayadhibiti vilivyo na kisha kuleta faida.

Kwa kuzingatia hayo, mfanyabiashara au mjasiriamali anapaswa kujua namna ya kupenya katika kipindi cha hali ngumu ili kuhakikisha kuwa anaibuka na ushindi katika biashara yake.

Hivyo ndivyo mfanyabiashara au mjasiriamali anavyotambulika. Wahenga wanasema `Bahari tulivu haizalishi nahodha hodari.'

Kumbe, ubora upo kwenye mawimbi, hofu, mkazo, wasiwasi, hasara na woga.

Mfanyabiashara yeyote mwenye uwezo wa kupenya katika mazingira ya hofu, woga, wasiwasi, hasara na mkazo, huibuka na kupata tuzo ya ubora katika mazingira ya biashara yake.

Hayo ndiyo mazingira pekee ya uaminifu ambayo hukuza biashara, kuongeza wateja na kuleta imani ambayo ni muhimu katika kufanya biashara kwa uhuru.

Jambo la msingi hapa ni kutambua kitu cha kufanya baada ya kutokea kwa hasara katika biashara.

Je; utajuaje kuwa hasara imetokea katika biashara yako. Ni lazima kichwa chako kiwe wazi kwanza kuhusu mazingira ya utokeaji wa hasara, ndipo usonge mbele katika kutafuta suluhisho.

Biashara kujiendesha kwa hasara ni pale matumizi yanapokuwa makubwa kuliko fedha inayoingia. Haya matumizi siyo lazima yawe mapya, yanaweza kuwa ni yale yale kama bili za umeme, maji, matangazo, mishahara na kadhalika.

Inawezekana matumizi yako hivyo hivyo (constant) lakini mara nyingi fedha zinazoingia, hazitabiriki hasa kwa biashara inayoanza. Hii inaweza kusababishwa na biashara kutokuwa na wateja wa kudumu, mabadiliko katika mahitaji na uelekeo wa masoko na ujuzi katika kufanya matangazo na mauzo.

Hata hivyo, hali hii haipaswi kuwa ya kudumu, mara nyingi ni ya mpito tu. Lakini kama biashara yako mara kwa mara inajikuta ikijiendesha kwa hasara, hapo ndipo unapotakiwa kujitafakari upya kuhusu namna ya kuendesha biashara

Tafuta ushauri wa kitaalamu na ikibidi usimamizi wa karibu kutoka kwa wataalam mbalimbali katika masuala ya biashara na usimamizi.

Ili kujua mazingira ya upatikana wa hasara katika biashara, lazima uone ukosefu wa fedha za kulipia gharama za uendeshaji ikiwemo meme, maji, mishahara, malighafi na matangazo nakadhalika. Hili linapofika, huo uwe mwanga mwekundu katika biashara yako na hatua za haraka lazima zichukuliwe.

Laki pia pale mazingira ya salio la kuendesha biashara lililopo benki au kwenye simu , lipokuwa sifuri au madeni ni makubwa zaidi na hujui namna ya kupandisha salio kufikia mahali pa kujimudu, ujue kwamba hapo umeingia hasara.

Hali hii inapotokea, lazima ufahamu kuwa si ya kawaida na kwa hiyo lazima utafute mbinu mbalimbali ikiwemo kuwaona wataalamu wa biashara ili wakupe ushauri mzuri wa namna ya kurudi katika hali nzuri.

Katika hali ya mauzo, ikiwa mauzo yako si yale yaliyopangwa katika mpango biashara wako, nalo ni tatizo linaloashiria hasara.

Huu mpango biashara ni muhimu kuwa nao kama mfanyabiashara makini kwa sababu ndiyo unobeba mipango na malengo yote biashara inayotakiwa kufikiwa ndani ya muda uliowekwa.

Mfanyabiashara au mjasiriamali yeyote anapokuwa kwenye mazingira ya hasara, kuna njia nyingi anazopaswa kuzichukuwa ili kukabiliana na matatizo hayo.

Tambua kuwa kuna umuhimu wa kuweka mipango mingi ya namna ya kukabiliana na mazingira ya hasara.

Hata hivyo, jambo la muhimu zaidi ni kujiandaa kisaikolojia kwamba hasara ipo kwenye biashara na inaweza kutokea muda wowote. Matarajio yasiwe makubwa kuliko uhalisia, kwa sababu ushindwa tu.

Kama unadhani mambo yatakwenda vizuri na mipango yako uliyoiweka kukabiliana na hali ngumu, basi siku mambo yakienda tofauti, utakuwa katika wakati mgumu zaidi kuliko ilivyotarajiwa.

Pili, tafuta namna ya kurudisha nguvu kutoka katika mazingira ya hasara na kuwa mazingira ya faida.

Nyakati ngumu na hasara kwenye biashara, huumiza sana moyo, hudidimiza juhudi na kukatisha tamaa. Lakini kamwe nyakati hizi hazidumu na kwa hiyo lazima mjasiriamali lazima asimame imara.

Kwa kuzingatia hali hiyo, unaweza kujipa mapumziko au kujiweka mbali na mazingira ya kazi kwa muda, huku ukitafakari kilichokukwamisha na hatua za kuchukua ili kukabiliana na changamoto hizo.

Matumizi ya vileo na kujihusisha kwenye starehe mbalimbali si mazuri katika hili.

Usifanye maamuzi kwa hisia, ukiwa kwenye hali ya shinikizo huku ukiandamwa na hasara katika biashara, vinginevyo utajikuta ukiwa na hasira, huzuni, woga na hofu.

Huu si wakati wa kufanya uamuzi hasa unaohusu biashara. Tulia na tafuta suluhu kupitia watalaam au marafiki wema.

Katika mazingira ya hasara ndani ya biashara, unatakiwa kujitahidi kuwa na mtandao saidizi.

Hapa ni kuangalia jumla ya watu wote unaokutana nao kila siku katika shughuli za kibiashara na kazi. Hao wanapaswa kuwa wasaidizi wako utakapowahitaji. Unapaswa kuwa na watu ambao ni nyenzo kuu na ujaribu kuwaepeka wale ambao ni mzigo.

Jambo la msingi katika kukwepa hasara, ni kutathmini hali halisi ya maisha yako.

Hasara ni funzo moja zuri katika maisha ya biashara imara. Ni nafasi yako kujifunza wapi ulikosea na nini unapaswa kufanya ili uzalishe faida tu.

> **Baadhi ya nchi hazitaki kuona mazungumzo ya amani yanafanikiwa, Hawajali maisha ya Waukraine wanaopoteza maisha yao wala athari wanazozipata watu wa Ulaya...**

Utumie vizuri wakati huu kufanya uchambuzi yakinifu.

Pia jitahidi kujiepusha kuishi katika mazingira ya hasara, katika historia hakuna mtu ambaye alifanikiwa sana na hakupata hasara.

Kila shujaa unayemjua na mafanikio yake., kuna wakati fulani alishapata hasara. Kinachomfanya mtu kuwa shujaa ni uwezo wa kunyanyuka na kutoruhusu hasara kuathiri utendaji.

Ondoa dhana ya kuishi katika hasara kwa sababu hiyo inazua hofu na woga.

Ukiwa kama mfanyabiashara, unapaswa kutenganisha hasara ya biashara na utendaji wako binafsi. Ni ngumu mno kutenga mambo ya kibiashara na maisha binafsi.

Kama biashara yako imekumbana na hasara, unapaswa kujua kwamba hilo linahusu biashara na siyo familia nyumbani kwako au siyo wewe binafsi, ndugu au marafiki.

Kwa hiyo hupaswa kujilaumu wala kuwalaumu watu, jikite na biashara na hakikisha utendaji wa biashara hauathiri amani na utulivu ukiwa katika mazingira ya nje ya kazi.

Watu wengi wamejikuta wakiingia katika migogoro mikubwa kwenye ndoa, familia na marafiki kutokana na kuchanganya biashara na undugu.

Ni vitu visivyochangamana kamwe na umakini mkubwa unahitajika kiuweledi katika kusimamia misingi ya kibiashara katika mahusiano ya familia.

Mfanyabiashara anapaswa kujua kuwa mbinu bora zaidi ya kumshinda adui ni kumjua vizuri adui huyo.

Kamwe huwezi kupigana na adui usiyemfahamu vizuri.

Hivyo chukua muda kujua sababu za kupata hasara na nini ufanye hatimaye upate faida.

Mbinu bora kuliko zote ni kujifunza, vyovyote itakavyokuwa, maisha lazima yaendelee. Lakini kuendelea kujifunza ndiyo jambo muhimu ambalo unapaswa kulifanya mara zote.

Maisha ya mfanyabiashara ni mfululizo wa mafunzo yasiyokwisha. Hivyo usikaze mishipa ya shingo, jifunze kila inapobidi ili kujiimarisha.

Pamoja na yote, kila mtu ana namna yake ya kukabiliana na hali ngumu na hasara.

Hata hivyo, mbinu ulizozipata leo zimethibitishwa kitaalamu katika kuokoa biashara yoyote katika janga la hasara.






# Jipatie nakala ya **Jarida lako pendwa**


Leo ndiyo, kesho yetu.
Mwelekeo
AFYA
Nini kifanyike kukabili kisukari Afrika
Makala
Lissu amkubali Rais Samia
Asema anaonyesha mwelekeo mwema
HABARI NDANI
Serikali yamwaga mabilioni kwa barabara
Nini kitatokea Ukraine Feb. 24
Utepe, kiti maalum kutumika kuua mbu
Maajabu, mwili mmoja makaburi mawili

***Leo yetu ndiyo, Kesho yetu***

Follow / subscribe
umgdigital

www.umg.co.tz

# Karibu Balozi Dk. Chana katika sekta ya michezo

**Na Eleuteri Mangi, WUSM, Dodoma**

REJEA mabadiliko madogo ya Bazara la Mawaziri aliyoyafanya, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, Februari 14 mwaka huu ambapo alimteua, Balozi Dk. Pindi Chana kuwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo na kumuapisha Februari 15, mwaka huu Ikulu jijini Dar es Salaam kushika wadhifa huo mpya akitokea Wizara ya Maliasili na Utalii.

Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa sasa kipyenga kimepigwa ikiwa imepata Waziri mpya, Balozi Chana mwanadiplomasia na mwanasiasa ambaye anaendelea kuongoza sekta alizowahi kuhudumu ndani na nje ya nchi.

Akizungu za mara baada viongozi wapya kuapishwa na Rais Dk. Samia Ikulu jijini Dar es Salaam, Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango, amewasisitiza viongozi hao kuwa wanajua maadili ya kiserikali na kuwahimiza washirikiane na kubadilishana uzoefu ili kufikia malengo ya hayo.

Dk. Mpango anasema takwimu zinaonesha sekta ya utamaduni inakua kwa kasi kuliko sekta zote nchini na inaajiri vijana wengi ambao ni tegemeo la taifa la kesho.

"Mhe. Pindi Chana, ukaitendee haki, vijana wetu wanategemea sana hiyo sekta. Uwe na mashirikiano kati yako wewe na watendaji, mkae kama timu moja ya kuwaletea maendeleo Watanzania," anasema Dk. Mpango.

**BALOZI DK. PINDI CHANA NI NANI?**

Yeye ni mbobezi katika masuala ya Sheria mwenye Shahada ya Uzamivu (PhD) ya Sheria ya Chuo cha Mzumbe kuanzia 2010 hadi 2013, Shahada ya Uzamili ya Sheria ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (LL.M) kuanzia mwaka 2001 hadi 2003 na Shahada ya Kwanza ya Sheria (LL.B) mwaka 1994 hadi 1991 Chuo Kikuu cha Peoples Friendship (Lumumba) Moscow, Russia.

Kama hilo halitoshi, Balozi Chana amehudumu Ubunge katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa awamu tatu, mwaka 2005 hadi 2010, 2010 hadi 2015 na kuanzia 2020 hadi sasa. Nafasi hii ya Ubunge ndiyo imefungua njia kwa Balozi Chana kuaminiwa na Rais Samia na kumpa dhamana ya kuongoza wizara kadhaa na sasa yupo katika Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Kabla ya uteuzi huo, Balozi Chana amehudumu katika nafasi kama hiyo katika Wizara za Maliasili na Utalii kabla ya hapo alikuwa Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge).

Hadi sasa ni Mjumbe wa Kamati ya Katiba na Mambo ya Sheria, Wizara ya Mambo ya Katiba na Sheria, eneo ambalo anatumia vyema taaluma yake ya Sheria. Bila ya kusahau ameiwakilisha Tanzania nchini Kenya akiwa Balozi kuanzia mwaka 2017 hadi 2020.

Aidha, Waziri Chana amekuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Haki na Utawala Bora kuanzia mwaka 2010 hadi 2014, Mjumbe wa Baraza la Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya kuanzia mwaka 2012 hadi 2013, Mjumbe wa Baraza la Sanaa la Taifa kuanzia mwaka 2009 hadi 2013 na Kamishna wa Tume ya Pamoja ya Fedha kuanzia mwaka 2009 hadi 2013.

Kalamu yangu haiwezi kusahau kuwa yeye ni miongoni mwa wanasiasa wanawake Tanzania, amewahi kufanyakazi ya kusimamia taasisi za elimu nchini akiwa Mjumbe wa Baraza la Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili kuanzia mwaka 2008 hadi 2013 na Mjumbe wa Baraza la Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kuanzia mwaka 2009 hadi 2010.

Kwenye diplomasia, Balozi Chana amewahi kuwa Mwakilishi wa Kudumu wa Tanzania wa Umoja wa Mataifa Nairobi, nchini Kenya katika Shirika la Umoja wa Mataifa la Makazi (UN Habitat) na Mazingira (UNEP) mwaka 2017 na Katibu wa Chama Cha Mapinduzi Mahusiano ya Kimataifa 2016 na Mwenyekiti wa Mabalozi wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) Nairobi nchini Kenya kuanzia mwaka 2019 hadi 2020. Kazi alizofanya Waziri Chana zinamfanya awe na mawazo mapana ya kiuongozi ndiyo maana anapewa Wizara mbalimbali kutekeleza majukumu yake.

Waziri huyu ni mfano wa kuigwa, ana uzoefu wa kufanya kazi kuanzia ngazi ya chini ambayo ndiyo imekuwa njia mwafaka ya kuijua serikali na kuitumikia kwa moyo wake wote.

Alifanya kazi ya kuwa Mwanasheria wa Elimu ya Utafiti na Utunzaji wa Mazingira Tanzania Mwaka 2000 hadi 2010, Ofisa Sheria wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa kuanzia 2000 hadi 2005.

Vile vile amefanyakazi katika Kampuni ya Sheria ya Uingereza akiwa Katibu mwaka 1997 hadi 1999, amefanyakazi katika Benki ya Barclays, Uingereza mwaka 1995 hadi 1998, Kampuni ya Coca-Cola mwaka 1996 hadi 1997 na Mtangazaji wa Benki ya Urusi mwaka 1994 hadi 1995.




Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo Balozi Dkt. Pindi Chana (katikati) akikabidhi Kombe kwa timu ya Fountain Gate, baada ya kutwaa Ubingwa wa Ubingwa wa mashindano ya soka kwa Shule za Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), baada ya kuifunga timu ya Awaro kutoka Ethiopia, mabao 3-0 katika mechi iliyochezwa Uwanja wa Azam Complex Chamazi, Dar es Salaam. Na Mpigapicha Wetu

> **Kabla ya uteuzi huo, Balozi Chana amehudumu katika nafasi kama hiyo katika Wizara za Maliasili na Utalii kabla ya hapo alikuwa Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge).**



Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Balozi Dkt. Pindi Chana

# Burudani

## Diamond: Vijana tutafute pesa



**Na Mwandishi Wetu**

NYOTA wa muziki wa Bongo Fleva na Bosi wa Wasafi Media nchini, Abdul Nassib 'Diamond Platnumz amewataka vijana kutafuta pesa ili waweze kuonekana wa maana katika jamii.

Akizungumzia hilo kupitia kwenye ukurasa wake wa Instagram, Diamond alisema yeye asingekuwa na pesa hakuna mwanamke hata mmoja angempenda.

"Dada zangu hivi ningekuwa sina hela kweli mngenipenda? Hivi mnanipenda kuliko latifa au Nassib, si mnaona mimi nilivyo na uso mbaya, lakini kila demu ananiona 'handsome boy'. Wanaume tafuteni hela acheni braabraa," alisema Diamond.

## Rihanna atangaza kupata mtoto wa pili



**Na Mwandishi Wetu**


MSANII wa muziki kutoka nchini Marekani, Rihanna kwenye show yake wakati wa mapumziko katika mchezo wa fainali wa Super Bowl kati ya Philadelphia Eagles dhidi ya Kansa City Chief, amethibitisha kuwa na ujauzito mwingine.

Huyo atakuwa mtoto wa pili kwa Rihanna, baada ya mwaka mmoja uliopita kupata mtoto wa kwanza na rapa kutoka Marekani, Asap Rocky.

Wengi wameshangazwa na usiri aliokuwa nao Rihanna ambaye majuzi kwenye mahojiano na waandishi wa habari, kabla ya mchezo hakuonesha ishara yoyote ya kuwa mjamzito bali alisema 'suprise' nyingi zitakuja.

## LeBron James awa mfungaji bora wa muda wote

**Na Mwandishi Wetu**




MCHEZAJI nyota wa kikapu nchini Marekani, LeBron James amekuwa mfungaji bora wa muda wote wa Ligi ya kikapu ya nchi hiyo NBA, akipita rekodi ya Kareem Abdul-Jabbar ya miaka 39. Nyota huyo wa Los Angeles Lakers, James "38" alifikisha pointi 38 katika kushindwa 133-130 na Oklahoma City Thunder na kuvuka alama ya Abdul-Jabbar ya 38,387. Awali Abdul-Jabbar, alivunja rekodi ya kufunga mabao Aprili 1984, miezi nane kabla ya James kuzaliwa. "Kuweza kuwa mbele ya gwiji na mtu stadi kama Kareem, ina maana kubwa sana kwangu," alisema James.

## Gigy Money aomba mahusino mazuri Mungu



**Na Mwandishi Wetu**

MSANII wa muziki na Video Queens mwenye vituko vingi nchini, Gift Stanford maarufu kama 'Gigy Money' amesema anaomba kuwa na mahusino mazuri na Mwenyezi Mungu, ili atimize ndoto zake. Akiweka wazi hilo kupitia kwenye ukurasa wake wa Instagram, Gigy Money alisema kila akifanyacho mwanadamu hana budi kumtanguliza Mungu mbele.

# MICHEZO KIMATAIFA




## Mwili mchezaji aliyefariki kwa tetemeko warudishwa Ghana, wazikwa

**ANKARA, Uturuki**

MWILI wa mchezaji Christian Atsu, aliyefariki katika tetemeko la ardhi lililotokea Uturuki wiki mbili zilizopita, umerudishwa nchini kwao Ghana. Ndege iliyobeba mwili wa marehemu ilitua mjini Accra, Ghana Jumapili jioni na jeneza lake lilibebwa na wanajeshi wa nchi hiyo.

Atsu alikutwa amefariki siku ya Jumamosi chini ya nyumba yake Kusini mwa Uturuki. Alikuwa akiichezea Klabu ya Hatayspor. Winga huyo aliichezea timu ya taifa ya Ghana mara 65 na kuisaidia timu yake kufika fainali ya Kombe la Mataifa ya Afrika 2015. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, a alichezea timu za Premier League ambazo ni Everton na Newcastle.

Akizungumza katika Uwanja wa ndege wa Kotoka katika mji mkuu wa Accra, Makamu wa Rais wa Ghana Mahamudu Bawmia alisema:



## Kipa afariki baada ya kudaka penalti

**BRUSSELS, Ubelgiji**

KIPA wa Klabu ya Winkel Sport B inayocheza Ligi Daraja la Pili nchini Ubelgiji, Arne Espeel (25) amefariki baada ya kudaka mkwaju wa penalti mwishoni mwa wiki iliyopita wakati timu yake ikicheza mchezo wa ligi hiyo.

Timu hiyo ilikuwa ikicheza mechi ya Ligi Daraja la Pili Magharibi mwa Brabant, ilikuwa mbele kwa mabao 2-1 dhidi ya Westrozebeke wakati wapinzani wao walipopata penalti kipindi cha pili. Kwa mujibu wa taarifa kutoka kwenye vyombo vya habari nchini Ubelgiji, Espeel aliokoa mkwaju huo wa penalti lakini akaanguka chini.

Hata hivyo alipatiwa huduma ya kwanza haraka kumsaidia, lakini ikaripotiwa kwamba alifariki muda mfupi akiwa njiani kupelekwa hospitali.

## Ubalozi Marekani wasaidia wasichana vifaa vya michezo

**Na Mwandishi Wetu**

ZAIDI ya wasichana 200 ambao ni wachezaji wa mpira wa miguu, watanufaika moja kwa moja na msaada wa vifaa vya michezo vyenye thamani ya dola za Marekani 8,200 kutoka Ubalozi wa Marekani nchini, kupitia programu yake Ruzuku Ndogo ya Diplomasia ya Umma.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Ubalozi wa Marekani nchini, vifaa hivyo ni sehemu ya mradi wa Michezo kwa Wasichana, unaotekelezwa na Asasi isiyo ya Kiserikali ya Kuwawezesha Wanawake ya Zanzibar (WEZA) kwa ushirikiano na Ubalozi wa Marekani.

Taarifa hiyo ilisema mradi huo, unatumia michezo kuwajengea uwezo wasichana, kuwasaidia kutimiza ndoto zao kwa kushiriki katika mazoezi ya viungo, shughuli za michezo ya kitimu, elimu ya afya na mafunzo ya stadi za maisha.

Katika hafla ya kukabidhi vifaa hivyo, wachezaji walitambuliwa kama watu wa kuigwa wanaowahamasisha wasichana wengine kuingia katika michezo, huku wakikuza hadhi na kukubalika kwa wasichana katika jamii. Akizungumzia msaada huo, Ofisa wa Ubalozi wa Marekani anayeshughulikia masuala ya Umma, James Rodriguez aliwashukuru waandaji na washiriki kwa jitihada zao za kuboresha maisha na fursa kwa wasichana wa Zanzibar.

"Michezo ni zaidi ya mazoezi ya kimwili yanayoleta manufaa katika afya yako. Michezo hufundisha stadi muhimu za maisha kama vile ushirikiano, uvumilivu na ustahimilivu, mambo ambayo yanaweza kukusaidia sana maishani na kazini," alisema.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji na mwanzilishi mwenza wa WEZA, Petra Karume aliishukuru Serikali ya Marekani kwa msaada huo.

"WEZA inatambua manufaa ya kutumia michezo kuchanganya na vipengele vingine kama nyenzo ya maendeleo. Mradi wetu unashughulikia masuala mengi yanayowakabili watoto wa kike, kama vile kutokuwepo usawa wa kijinsia katika michezo, upatikanaji wa taarifa kuhusu afya na stadi za maisha," alinena.

Alisema Mradi wa Sports4Girls, unawasaidia wasichana wa Pemba na Unguja kwa kuwapatia vifaa na mavazi ya michezo yanayoendana na kukubalika katika utamaduni wa eneo hilo, mafunzo ya stadi za maisha, sodo zinazoweza kutumiwa zaidi ya mara moja na elimu ya afya.

# Simba: Hatujakata tamaa licha ya kufungwa

**Na Mwandishi Wetu**

WAWAKILISHI katika michuano ya Kombe la Afrika, Simba imesema haijakata tamaa licha ya kufungwa mabao 3-0 katika iliyochezwa Uwanja wa Mkapa jijini Dar es Salaam dhidi ya Raja Casablaca.

Akizungumza mwishoni mwa wiki mara baada ya mechi hiyo kumalizika Kocha Msaidizi, Juma Mgunda alisema kwa kuwa wamebakiza michezo minne miwli nyumbani na iwili ugenini watakikisha wanapigana kufa kupona hadi kupata nafasi ya kucheza robo fainali.

> **Mpira ni mchezo wa makosa hivyo walifanya makosa Jumamosi wapinzani wa...**

"Mpira ni mchezo wa makosa hivyo walifanya makosa Jumamosi wapinzani wao wakatumia nafasi ya ya kuwaadhibu mabao hayo ambao, Simba haijawahi kupoteza idadikubwa kama hiyo," alisema.

Mechi hiyo ni ya pili mfululizo kupoteza Simba kupoteza baada ya kufungwa bao 1-0 ugenini dhidi ya Horoya ya nchini Guinea ambazo ziko Kundi B.

Katika mechi hiyo mshambuliaji, Hamza Khaba alifungia Raja bao la kwanza dakika ya 30 akimalizia pasi ya kiungo Zakaria Habti.

Naye Soufiane Benjdida akafunga la pili dakika ya 82 akimalizia pasi ya mshambuliaji mwenzake, Mmorocco Mohamed Al Makahasi.

Aliyehitimisha shangwe za mabao ya Raja ni beki, Ismail Mokadem kwa kufunga la tatu kwa penalti dakika ya 86 baada ya beki Mkenya, Joash Onyango kuunawa mpira kwenye boksi.

Raja inafikisha pointi sita na mabao nane ya kufunga bila kuruhusu hata bao moja ndani ya mechi mbili baada ya kuilaza Vipers ya Uganda mabao 5-0 kwenye mechi ya kwanza Casablanca.

Simba SC inakamilisha mechi mbili bila ushindi kufuatia kuchapwa bao 1-0 na wenyeji, Horoya Jijini Conakry nchini Guinea. Horoya nayo baada ya kutoka suluhu na wenyeji Vipers wanafikisha pointi nne na wanaendelea kukamata nafasi ya pili, wakati Simba inashika mkia.

## Dk. Mabula: Wasanii tumieni ujuzi wenu kuelimisha jamii

**Na Mwandishi Wetu, Mwanza**



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dkt. Angeline Mabula

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dkt. Angeline Mabula ametoa rai kwa wasanii wilayani Ilemela mkoani Mwanza kutumia ujuzi wao kuelimisha na kukemea maovu katika jamii.

Dkt. Mabula altoa rai hiyo wakati akizungumza na wasanii hao katika Tamasha la Wasanii wa Wilaya ya Ilemela, lililofanyika Februari 19, mwaka huu Uwanja wa CCM Kirumba jijini hapa.

Alisema, zamani nyimbo na filamu zilikuwa zinalenga kuelimisha jamii hivyo wasanii hao wanaojishughulisha na vitu mbalimbali watumie ujuzi wao na kuuelekeza kwenye kuelimisha, kukemea maovu na kuhamasisha jamii iwe wa moja.

"Watanzania ni wamoja, nani kisiwa cha amani watu wanakuja kujifunza hapa, tumieni filamu, kalamu zetu, utamaduni wetu kama zitakuwa na maudhui yanayojenga umoja, ukiangalia nyimbo za zamani pamoja na filamu nyingi zilikuwa zinalenga kuelimisha jamii".

Alahidi kuwapatia kompyuta mpakato 'laptop' kwa ajili ya wasanii hao kufanyia shughuli zao za uzalishaji pamoja na pikipiki kwa ajili ya usafiri.

Pia aliwashauri wasanii hao ili waweze kupata fursa mbalimbali za kiuchumi na serikali, iwatambue warasimishe shughuli wanazofanya. Alisema serikali imetenga sh. bilioni mbili kwa ajili ya wasanii, hivyo jukumu lao ni kuandika andiko vizuri na lieleze vitu watakavyoenda kufanya na namna watakavyorejesha.

"Rasilimisheni shughuli zenu au biashara mnazozifanya, ili muweze kufanikiwa lakini pia mjiunge katika Shirikisho na Bodi ya Filamu itawatambua na kuwakopesha fedha kutoka kwenye mfuko wa sanaa hivyo mtapata mitaji".

Kwa upande wake Katibu wa Chama cha Waigizaji Tanzania (TDFAA) Wilaya ya Ilemela, Malamala Shunashu, chama hicho kina jumla ya vikundi 54-58 katika kata 19 za Wilaya ya Ilemela huku changamoto walizonazo ikiwa ni pamoja na kutokuw]a na ofisi ya chama, vifaa vya uendeshaji na uzalishaji wa filamu.

"Changamoto za kiuchumi ambapo wasanii na wadau wote inatuwia vigimu kufanya uzalishaji wa filamu, warsha, mikutano, makongamano, semina, mafunzo na kukutana na wadau wakongwe na wazoefu katika tasnia hii kwa ajili ya kubadilisha uzoefu kwani hata yote yamekua yakifanyika mkoani Dar es Salaam na kwingineko na si Mwanza alisema".

## Nabi aelezea siri ya ushindi dhidi ya TP Mazembe

**Inatoka Uk.24**

Akizungumza mara baada ya kumalizika mchezo huo kocha huyo alisema, wameshinda kutokana na kuwa kundi kubwa la watu licha ya kwamba waliwakosa wachezaji wao muhimu, Fiesal Salum 'Fei Toto' aliyeomba kuvunja mkataba na Bernad Morison. Hata hivyo alisema hana kinyongo na Feisal, kama ataamua kurudi yeye kama yeye kwa kuwa ni mchezaji mzuri hivyo ataendelea kuimarisha kikosi.

Katika mechi ya juzi mabao ya Yanga yalifungwa na mshambuliaji raia wa Zambia, Kennedy Musonda dakika ya saba, kiungo Mudathir Yahya dakika ya 11 na winga Mcongo, Tuisila Kisinda dakika ya 90, wakati la Mazembe likifungwa na Alex Ngonga kwa mpira wa adhabu dakika ya 80.

Yanga SC inaokota pointi tatu za kwanza katika kundi hilo, baada ya kuchapwa 2-0 kwenye mechi ya kwanza wiki iliyopita na wenyeji, Monastir nchini Tunisia, wakati Mazembe inapoteza mechi ya kwanza ikitoka na kushinda 3-1 nyumbani dhidi ya Real Bamako ya Mali.

Mechi nyingine ya Kundi D, Real Bamako ililazimishwa sare ya 1-1 na Monastir Jijini Bamako nchini Mali.

Monastir inaendelea kuongoza kundi hilo kwa pointi zake nne ikifuatiwa na Yanga na Mazembe zenye pointi tatu kila moja, wakati Real Bamako yenye pointi moja inashika mkia.

Mechi zijazo Februari 26, Yanga watakua wageni wa Real jijini Bamako na Mazembe watawakaribisha Monastir jijini Lubumbashi.

## Waziri Mkuu: Iungeni mkono Namungo kwa dhati

**Inatoka Uk.24**

na kuinua hali za kiuchumi kupitia biashara zinazofanywa na wajasiriamali wadogo na wakati.

Majaliwa aliyasema hayo wakati akizungumza na wadau wa michezo katika Ukumbi wa Mikutano wa Chama cha Walimu Wilaya ya Ruangwa (CWT) na kuongeza kuwa ni vizuri wote wakaungana kuishabikia na kuiunga mkono Namungo kwa hali na mali.

"Kama siy Namungo FC, nani alitegemea Ruangwa leo ingekuwa na uwanja ambao unatumika hadi kwa mechi za usiku. Au nani angeamini kuwa miamba ya soka nchini Yanga, Simba na Azam ingetembelea Ruangwa na kutoa burudani kwa wana Ruangwa?" Alihoji Waziri Mkuu.

Majaliwa alitoa mfano wa timu kadhaa zilizokuwa maarufu nchini, lakini leo hazipo na mikoa ambako zilikuwepo hakuna tena timu za Ligi Kuu na imekuwa ngumu kwa timu hizo kupanda tena ngazi hiyo.

Kiongozi huyo ambaye ni mdau mkubwa wa michezo hususan soka hapa nchini alisema kwa vyovyote iwavyo, uwepo wa Namungo FC na ujio wa timu 15 za Ligi Kuu ya NBC, kumeinua hali ya uchumi wilayani humu na kusisitiza kuwa kila mdau wafanye kila analoweza ili kuhakikisha timu hii inaendelea kubaki Ligi Kuu.



## Diamond: Vijana tutafute pesa

Uk. 22

Leo yetu ndiyo kesho yetu

# Mwelekeo Spoti

| Jumanne Januari 25, 2013 |



## Kipa afariki baada ya kudaka penalti

Uk. 22



## Waziri Mkuu: lungeni mkono Namungo kwa dhati

**Na Abdul Mitumba, Ruangwa**

MBUNGE wa Ruangwa na Waziri Mkuu wa Tanzania, Kassim Majaliwa, amewakumbusha wadau wa michezo hususan soka wilayani Ruangwa, kuona umuhimu wa kuiunga mkono kwa dhati timu ya Namungo ili isishuke daraja kwa sababu uwepo wake una faida kubwa kwao kijamii na kiuchumi.

Aidha, Majaliwa amesema hivi sasa Ruangwa inajulikana maeneo mengi si kwa sababu tu yeye ni Waziri Mkuu, bali hata uwepo wa Namungo FC umechangia kuitangaza wilaya na kuiongezea wageni wanaotembelea Ruangwa

Inaendelea Uk.23



# Nabi aelezea siri ya ushindi dhidi ya Mazembe

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Nasrideen Mohamed amesema ushindi wa mabao 3-0 katika mchezo wa Kombe la Shirikisho la Afrika dhidi ya TP Mazembe ni kutokana na kupoteza mechi yao ya kwa ambayo ilifungwa mabao 2-0 na Monastir. Inaendelea Uk.23



Mshambuliaji wa Yanga, Jesus Moloko, akimtoka mmoja wa mabeki wa TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, katika mechi ya michuano ya Kombe la Shirikisho la Afrika iliyochezwa mwishoni mwa wiki Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaa. Picha na Fullshangwe



## Simba: Hatujakata tamaa licha ya kufungwa

HABARI UK.23